Jumatatu Septemba 7, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580331

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 11



## Wazazi mbaroni tuhuma kumwozesha mwanafunzi


UKURASA 8

# Mchuano wazidi kupamba moto

• **JPM** aja na mambo 5 Kanda ya Ziwa, Lissu aahidi neema korosho, gesi Kusini, Zitto afunguka...*Uk. 2,3*



Tundu Lissu



John Magufuli



Zitto Kabwe

## 'Shamba boi' jela miaka 30 kwa kubaka mtoto wa bosi

UKURASA 4

## Atoka Muhimbili baada ya kukaa kwa siku 490

UKURASA 4

Scan Hapa




Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play
Download on the App Store

Fursa kwa Wagombea! 2020

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

VOTE

Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza katika kongamano maalum lililoandaliwa na Kituo cha Radio cha Safina la kuliombea Taifa katika uwanja wa Magereza, Kisongo jijini Arusha jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Ahadi 5 za JPM Kanda ya Ziwa

**Na Gwamaka Alipipi,**
MWANZA

ZIKIWA zimepita siku 10 tangu mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, kuzindua kampeni zake, ameshatoa ahadi kubwa tano kwa wananchi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa, atakazozitekeleza katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Dk. Magufuli alizindua kampeni za urais Agosti 29, mjini Dodoma, baadaye kuanza safari ya kutafuta kura katika mikoa ya Singida, Tabora, Shinyanga, Simiyu, Mara, leo anatarajia kuzungumza na wananchi wa Mkoa wa Mwanza.

Akiwa katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, Dk. Magufuli alitoa ahadi ya kujenga viwanda, barabara za lami, shule, ununuzi wa meli pamoja na kufikisha huduma ya umeme na maji vijijini.

Akiwa mkoani Shinyanga, Dk. Magufuli aliwahakikishia wananchi wa mkoa huo kuwajengea kiwanda cha kuchakata pamba, lengo kuu likiwa ni kuhakikisha wakulima wanaongeza kipato, pamoja na fursa za ajira. "Nataka wakulima wa pamba muuze mazao yenu hapa hapa...nataka tutengeneze nguo hapa kisha tukauze Ulaya, sitaki tusafirishe malighafi nje halafu tuletewe nguo kwa pamba tuliyozalisha wenyewe," alisema Dk. Magufuli.

Aligusia Ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025, ambayo sehemu kubwa inaelezea maisha ya wakulima na wafugaji, hususani wananchi wa mkoa wa Shinyanga.

Pia, alisema atahakikisha vyama vya ushirika mkoani humo vinaimarika na wananchi wa mkoa huo kuwajengea vituo vya kuchakata na kuhifadhia mazao. Aliahidi kujenga kiwanda cha nyama mkoani humo pamoja na mikoa mingine, lengo likiwa ni kuwawezesha wafugaji kuuza nyama na kujipatia kipato.

"Katika ukurasa wa 45 wa Ilani ya CCM, inazungumzia kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, wananchi wa Mkoa wa Shinyanga ni wakulima wazuri wa kilimo cha pamba, hivyo mtaweza kuuza mazao yenu, kikubwa ndugu zangu naomba kura," alisema Rais Magufuli. Aliwahakikishia wakazi wa Shinyanga kuanzishwa kwa miradi ya ujenzi wa mabwawa ya kufugia samaki na ujenzi wa mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya binadamu, mifugo na kilimo mkoani humo na maeneo mengine yenye ukame.

Pia, ujenzi wa viwanda vidogo vya ngozi mkoani humo, vitakavyoongeza upatikanaji wa ajira.

Akiwa wilayani Bariadi mkoani Simiyu, Dk. Magufuli aliahidi wananchi wa mkoa huo kuwajengea daraja la Simiyu-Mwanza katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Vilevile, aliwaahidi upanuzi wa uwanja wa ndege mkoani humo, kuimarisha huduma ya afya ya mama na mtoto kwa kuzingatia vipaumbele vya Matokeo Makubwa Sasa (BRN), kwa kuzijengea uwezo zahanati na vituo vya afya.

Vilevile, aliahidi kufikisha umeme katika vijiji ambavyo bado havijafikiwa, na miundombinu ya maji na ujenzi wa shule za sekondari na msingi.

Akiwa wilayani Musoma mkoani Mara, Dk. Magufuli aliwaahidi wananchi wa mkoa huo kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, uliokuwa umesimama kwa zaidi ya miaka 20. Alisema Sh. bilioni 15 zimeshatengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo na itakuwa na uwezo wa kutoa matibabu ya figo.

Aliwaahidi wakazi wa mkoa huo, kuwajengea barabara kutoka Musoma hadi Busekera, yenye urefu wa kilometa 92 kwa kiwango cha lami.

Vilevile, aliwaahidi upanuzi wa uwanja wa ndege, akieleza kuwa hadi sasa wananchi 37 kati ya 87 wameshalipwa fidia ili kupisha upanuzi huo.

## Mgombea urais DP aahidi ruzuku kwa vyama vyote

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha Democratic (DP), Philipo Fumbo, amesema wananchi wakikipa chama hicho ridhaa kushika madaraka, serikali yake itatoa ruzuku kwa vyama vyote vya siasa vyenye usajili ili viweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Akizungumza jana katika mahojiano maalum na gazeti hili, alisema utaratibu wa kutoa ruzuku kwa ubaguzi ndiyo umefanya baadhi ya vyama kushindwa kuanza kampeni kwa wakati kwa sababu havina pesa.

"Leo unatunyima ruzuku sisi DP wakati chama chetu kimesajiliwa tangu mwaka 2002, haya ni maajabu kabisa, serikali yangu nitakayoiongoza itatoa ruzuku kwa vyama vyote bila kubagua," alisema.

Alisema ruzuku hiyo itatolewa kwa makundi mawili, kundi la kwanza itakuwa sawa sawa kwa vyama vyote vyenye usajili wa kudumu ili kuonyesha usawa kwa vyama vyote.

Fumbo alisema ruzuku ya pili itatolewa kutokana na uwingi na idadi ya kura, na hakuna kura itakayokosa ruzuku hata kama chama kimepata kura mbili.

"Hii ndiyo itakayokuwa misingi ya demokrasia ya kujenga chama, lakini leo vyama vinapokea ruzuku na vingine havipokei, wakati vingine havina muda mrefu tangu vimeanzishwa, hiki ni kiini macho cha demokrasia," alisema.

Aliongeza kuwa mambo mengine ambayo serikali yake itayawekea mkazo ni rasilimali ya nchi kumilikiwa na wazawa.

# Zitto ataja sababu wagombea ACT-Wazalendo kuenguliwa

**Na Enock Charles**

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ameeleza sababu 15 zilizotumika kuwaengua wagombea wao katika nafasi za ubunge na udiwani, na kwanini hawakubaliani nazo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Zitto alisema ili uchaguzi ufanyike kwa amani na utulivu, ni muhimu haki ikatendeka na ushindani ukafanyika ndani ya sanduku la kura na si vinginevyo.

Alizitaja baadhi yake ni wagombea walioandika barua kwa waajiri wao kuenguliwa kwa kigezo cha kutopatiwa ruhusa, jambo ambalo alidai siyo kweli kwa kuwa chama hicho kina uthibitisho wa barua za ruhusa walizopatiwa wagombea wao kabla ya kuanza kwa mchakato wa kuchukua fomu.

Nyingine ni baadhi ya wasimamizi walioghushi mapingamizi ambayo hayajaandikwa kabisa na wagombea katika eneo husika kutoka miongoni mwa vyama vinavyogombea hasa kwa upande wa Zanzibar.

Alisema wapo wasimamizi waliokataa kutoa au kupokea fomu za mapingamizi, waliofunga ofisi na kurudi mwishoni wakati ambao ni vigumu kwa wagombea wao kukamilisha taratibu zote.

Aidha, sababu nyingine wasiyokubaliana nayo ni baadhi ya wasimamizi kukataa kupokea picha za wagombea kisha kuwaengua kwa kigezo cha kukosa picha kwenye fomu na baadhi yao kutokutoa sababu za kuwaengua.

Pia, baadhi ya wasimamizi kubuni mapingamizi nje ya yale yaliyoainishwa kwenye kanuni na maelekezo ya uchaguzi. Alitolea mfano kutaka udhamini wa Katibu Mkuu wa chama taifa, ambapo wagombea kwa mujibu wa kanuni hawawezi kudhaminiwa na makatibu wa chama ngazi ya wilaya.

Kadhalika, Zitto alidai kuwa baadhi ya wasimamizi kubadilisha maandishi ya fomu za wagombea na kukataa baadhi ya wadhamini licha ya kwamba wamo kwenye daftari la kudumu la wapigakura.

Nyingine ni wasimamizi wa uchaguzi kutowateua baadhi ya wagombea kwa kigezo cha chama husika "kutosajiliwa" kwenye wilaya husika, kukataa mihuri halali ya Mahakama, kukataa mihuri halali ya chama hicho na kufanya maamuzi kabla ya wagombea kupewa pingamizi au kabla ya kurejesha majibu ya pingamizi.

Pia, yapo madai ya wasimamizi wa uchaguzi kupokea mapingamizi nje ya muda na kuwaengua wagombea kwa kigezo cha kushtakiwa na si kuhukumiwa na kutiwa hatiani kama sheria inavyosema, hivyo kuwanyima fursa ya kugombea nafasi za ubunge na udiwani kwa sababu zilizo kinyume cha sheria.

**MSIMAMO**

Zitto alisema msimamo wa chama hicho ni kuitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuchukua hatua dhidi ya dosari zote zilizojitokeza ili kuepusha migogoro kati ya wasimamizi wa uchaguzi na wananchi.

**AWAONYA POLISI**

Zitto alilionya Jeshi la Polisi kutojiingiza katika mkumbo wa siasa, na kuwa chanzo cha mtafaruku badala yake wafanye kazi zao kwa weledi bila msukumo.

"Tulitarajia Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, angesisitiza umuhimu wa haki, lakini katika hotuba yake nzima hajazungumzia haki," alisema Zitto.

Septemba mosi, mwaka huu, NEC, ilisema imepokea mapingamizi 557 kwa wagombea ubunge na udiwani kuhusu uteuzi wa wagombea wa nafasi hizo, na kwamba imeshaanza kuyafanyia kazi na watatoa uamuzi mapema iwezekanavyo.

## HABARI KITAIFA

## RC aagiza mgodi kuendelea kuchimbwa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, ameiagiza kampuni ya uchimbaji makaa ya mawe ya Market Insight Limited kuanza kazi mara moja ya uchimbaji katika Kata ya Ruanda wilayani Mbinga.

Kampuni hiyo ilisimamisha kazi ya uchimbaji madini ya makaa ya mawe tangu Desemba 2019 kutokana na mgogoro kati ya wabia wa uchimbaji wa madini hayo hali iliyosababisha Mndeme kuunda timu ya uchunguzi wa mgogoro huo iliyofanyakazi kwa siku 14.

Akitoa maagizo hayo kwa wadau wa madini ofisini kwake mjini Songea, Mndeme aliuagiza uongozi wa kampuni hiyo kuanza uzalishaji wa makaa ya mawe kuanzia Septemba 4, 2020 na kuhakikisha wanalipa madeni yote wanayodaiwa na serikali.

"Mnadaiwa mrabaha wa zaidi ya shilingi milioni 274, deni hili lilipwe mara moja kuanzia leo, na deni la kodi ya huduma mnalodaiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga lilipwe mara moja," alisisitiza.

Mndeme pia ameagiza madeni mengine ya kodi ambayo kampuni hiyo inadaiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalipwe kuanzia sasa na ameagiza Mhandisi wa Madini wa Kampuni ya Market Insight Limited, Fredrick Mwaipopo, ambaye anadaiwa kutuhumiwa kukimbia na shilingi milioni 62 za mishahara ya wafanyakazi wa mgodi atafutwe ili kujibu tuhuma hizo.

Mndeme ameiagiza kampuni hiyo kuanza kuuza makaa ya mawe kwenye viwanda vya ndani, ili kupata nishati ya kutosha na ziada inayobaki isafirishwe kwenda nje ya nchi.

Mndeme pia aliagiza kampuni hiyo kutoa ajira kwa Watanzania, kuchimba makaa ya mawe yenye viwango, ili soko lipanuke pamoja na kuzingatia afya za watu wote wanaofanya kazi katika mgodi huo na usalama wa mazingira ya mgodi huo.

Aliwaasa wasimamizi wa mgodi huo kutokuwa na migogoro, na kwamba wanapotofautiana wamalizane wao kwa kwao chini ya usimamizi wa ofisa madini wa mkoa.

Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Cosmas Nshenye, aliutaka uongozi wa kampuni hiyo kutekeleza maagizo yote ya serikali yaliyotolewa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, ikiwamo kupima afya za wafanyakazi wanaofanya kazi katika mgodi huo, kuwapatia vifaa vya usalama kazini vikiwamo barakoa na buti.

Naye Kaimu Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Ruvuma, Jumanne Mohamed Nkana, aliahidi kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa pamoja na kuitaka Kampuni ya Market Insight Limited kutekeleza maagizo hayo, na kwamba wakiendelea na migogoro, watachukuliwa hatua ikiwamo kunyang'nywa leseni za uchimbaji wa madini.



Wafanyakazi wa kiwanda cha kutengeneza mabomba cha Tanzania Steel Pipes Limited (TSP), ambao ni wanachama wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO), tawi la kiwanda hicho, wakiwa katika mkutano wa kujadili mambo mbalimbali yanayohusu maslahi yao, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Lissu aahidi neema gesi, korosho Kusini

**Na Mwandishi Wetu**

MGOMBEA ubunge wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema kuwa akipewa ridhaa ya kuongoza taifa atahakikisha wananchi wa mikoa ya kusini inayotoa raslimali ya gesi wananufaika nayo, huku akiahidi uhuru wa kuuza korosho.

Aidha, alisema serikali ya CHADEMA itahakikisha wananchi wanakuwa na uhuru wa kuuza korosho, ufuta, mbaazi na mazao mengine katika masoko wanayoona yana bei kubwa.

Lissu aliyasema hayo jana wakati akihutubia mamia ya wananchi wa mkoa wa Mtwara katika mkutano uliofanyika Mtwara Mjini.

"Tunataka watu wote wawe na haki sawa, kama wewe ni mkulima korosho na kuna bei kubwa India, Comoro kwanini mkulima azuiwe kuuza? Kwanini iwe ruhusa kwa wafanyabiashara kuuza bidhaa zao, lakini mkulima ananyimwa?" Alihoji.

"Tunataka kuwa na uhuru wa kufanya shughuli za kiuchumi, ili kila mtu apate faida, tutaweka utaratibu wa mtu kuuliza mazao yake anapoona kuna bei kubwa, nchi hii ni ya mfumo wa biashara huria, tutaondoa usumbufu kwenye mazao mengine ya mbaazi na ufuta ili wanufaike," alisema.

Alisema serikali ya CHADEMA ni ya uhuru, haki na maendeleo ikiwa na maana kwa mikoa ya Kusini kuweka mazingiara ya kuwa huru ili kufanya kazi halali na kupata riziki.

Lissu alisema kwa miaka mitano korosho limekuwa zao linaloiingiza taifa fedha za kigeni kuliko zao lolote la biashara hata yakijumlishwa yote.

Alisema ndani ya miezi ya kwanza ya serikali ya CHADEMA atafuta vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo na kwamba vitambulisho vinapaswa kutolewa bure.

Alisema uzalishaji wa gesi na mafuta una gharama za uharibifu wa mazingira, na kwamba ni lazima wananchi wa maeneo ya uzalishaji wa raslimali wapate faida na wawe wa kwanza kunufaika. "Tutatengeneza utaratibu wananchi wanaoishi mahali kuliko na rasilimali au utajiri wa asili, wananchi wanufaike wa kwanza na utajiri ambao Mungu ameweka," alisema.

"Wataita ubaguzi, lakini si ubaguzi kwamba nikilima pamba au korosho nikilima niwe wa kwanza kunufaika... kwamba dhahabu iko nyumbani kwangu nisiwe wa kwanza kunufaika nayo, ni muhimu niwe wa kwanza kunufaika," alisema.

Kwa mujibu wa Lissu, serikali ya CHADEMA itahakikisha Kusini inakuwa kitovu cha uchumi wa gesi ambao utaiwezesha nchi kuwa ya maendeleo, vinginevyo ni kuendelea kuwa maskini.

"Ndugu zangu wa Kusini suala la gesi CHADEMA ina jibu lako, hatutaki laana ya neema ya rasilimali ndani ya nchi yetu, hatutaki watu wateseke wakati maeneo yao yana utajiri mkubwa," alisema.

# Majaliwa ahakikisha mazingira mazuri uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imeandaa mazingira mazuri ya kuwawezesha Watanzania kujikwamua kiuchumi wakiwamo wafanyabiashara wadogo.

Alisema hayo jana, alipohutubia mkutano wa kampeni uliofanyika katika Kata ya Kirima Juu, wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro wakati akimwombea kura Rais Dk. John Magufuli na mgombea ubunge wa Jimbo la Moshi Vijijini, Profesa Patrick Ndakidemi na wagombea udiwani. "Nimekuja hapa kuwaomba sana kura yenu ya ndio kwa Rais Dk. Magufuli kwani mkiwa sehemu ya Watanzania mnafahamu kazi kubwa ya kupeleka maendeleo aliyoifanya nchi nzima bila ya ubaguzi wa aina yoyote, tuhakikishe tunampigia kura nyingi ili akaendeleze kazi aliyoianza."

Pia Majaliwa amesema Serikali ya CCM imejenga miradi mingi ya kimkakati ikiwamo ya afya, maji, elimu, umeme, barabara, viwanja vya ndege kwa ajili ya kuboresha maendeleo ya Watanzania. Serikali imetengeneza fursa katika maeneo mbalimbali zilizowezesha wananchi kujikwamua kiuchumi. Akizungumzia miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na serikali katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Waziri Mkuu alisema jumla ya Sh. bilioni 2.1, zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya Uru Kyaseni, Uru Kusini na Okaoni pamoja na upanuzi na ukarabati wa zahanati za Kahe, Kilema, Kisao, Chemchemi, Mowo, Kitowo na Kituo cha Afya Shimbwe. Pia, Sh. bilioni 12.2 zilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Kuhusu elimu msingi bila ada, Majaliwa alisema serikali imetoa Sh. bilioni 4.8 kwa ajili ya ukarabati, utawala, michezo, mitihani na posho kwa maofisa elimu kata na walimu wakuu katika shule za msingi 252 kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

"Serikali imetoa Sh. bilioni 10.2 kwa ajili ya fidia ya ada, chakula kwa shule za bweni na posho ya madaraka kwa wakuu wa shule katika shule za sekondari 59 kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Moshi."

Alisema Sh. bilioni 1.6 zimetumika kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 18, matundu ya vyoo 109, bwalo moja, nyumba sita za walimu na jengo moja la utawala na ununuzi wa mashine ya kudurufu mitihani katika shule za msingi Maweni, Mahoma, Ngaroni na Saghana.

Pia, alisema Sh. bilioni 7.3 zimetumika kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 26, matundu vyoo 45, maabara 14, mabweni sita na ujenzi wa nyumba za walimu katika shule za sekondari za Ashira, Umbwe, Sakayo Mosha na Muungano, Kisarika, Shimbwe na Kimochi.

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**ANNA ERNEST MWAKOSYA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **TOYOTA VANGUARD** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T101 DGE.** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA **POLISI: MTW/MTW/RB/6532205/2020.**

115887802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;247/2020**

**Ombi la ASHA ALLY ALMAS,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ALLY ALMAS MAUNDUMULA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 14/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 01/09/2020.

Tarehe 01/09/2020

Sahihi ya Hakimu

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

115887902

## Jela miaka 30 kubaka mtoto wa tajiri yake

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi, imemhukumu kijana Athumani Mussa wa Kata ya Milola, mkoani humo kutumikia kifungo cha miaka 30 jela, baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka mtoto wa mwajiri wake mwenye umri wa miaka 14 (Jina limehifadhiwa).

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu wa Mahakama hiyo, Muyonga Magala, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mshtakiwa aliulizwa iwapo anazo sababu zitakazomsaidia asipewe adhabu kali kwa kosa linalomkabili, hivyo aliomba asipewe adhabu kali kwa madai ni mkosaji wa mara ya kwanza na kuahidi kutorudia kosa la aina hiyo tena.

Baada ya utetezi huo, Mwanasheria wa Serikali, Godfry Mramba, akaiomba Mahakama kumpatia mshtakiwa adhabu kali, ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya kushiriki mapenzi na wasichana wadogo.

Mramba alidai kuwa kitendo cha mshtakiwa kushiriki mapenzi na watoto walio na umri chini ya miaka 18 ni kwenda kinyume cha sheria.

Hakimu Magala alimhukumu mshtakiwa adhabu hiyo kupitia vifungu (130) kifungu kidogo (1) na (2) (e) na 131 (1) kanuni ya adhabu sura ya 16 rejeo la mwaka 2019.

Awali, Mramba aliiambia Mahakama kuwa Apriri 03, 2020, eneo la Milola mshtakiwa akiwa ni mtumishi wa shamba la baba mzazi wa mwathirika, alimbaka mtoto huyo.



Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Sarah Msafiri (kushoto), akiangalia bidhaa za viungo vinavyozalishwa na Umoja Twaja Group, alipotembelea mabanda ya wajasiriamali wanawake katika kongamano la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa Maendeleo Endelevu lililofanyika Kigamboni jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni katibu wa kikundi hicho, Saleha Akhtar. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Aruhusiwa hospitali baada kulazwa mwaka na nusu

**Na Mary Geofrey**

MGONJWA Daudi Mikidadi (17), aliyekuwa amelazwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa siku 490, akisumbuliwa na tatizo la mapafu, ameruhusiwa baada ya hali yake kuimarika.

Mikidadi ambaye ni yatima anayeishi katika Kituo cha Children's Home Kurasini, alilazwa MNH kuanzia Aprili 20, mwaka jana, akiwa na tatizo la kushindwa kupumua vizuri.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Umma wa MNH, Aminiel Aligaesha, aliwaeleza waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuwa, kijana huyo baada ya kupokewa Muhimbili alikaa kwenye chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) kwa siku 127.

"Hospitali ya Taifa Muhimbili imemruhusu Daudi Mikidadi (17), kutoka hospitalini kwenda anakoishi na ataendelea kutumia mashine maalumu ya kumsaidia kupumua (oxygen concentrator), baada ya hali yake kuimarika," alisema Aligaesha.

Alisema, baada ya kumpokea uchunguzi ulifanyika na kugundua kuwa mapafu yote mawili yameharibika kutokana na kuugua aina moja ya ugonjwa mapafu (umehifadhiwa).

Alisema kutokana na ugonjwa huo atahitaji usaidizi wa mashine ya kupumulia kwa maisha yake yote au kupandikizwa mapafu yote mawili.

"Wataalamu wameridhika kwamba kwa hali aliyonayo sasa, anaweza kurudi kwenye kituo chake na Hospitali ya Muhimbili ikiendelea kushirikiana na kituo hicho kumpatia huduma za matibabu," alisema Aligaesha.

**MAHITAJI MUHIMU**

Aligaesha alisema, mbali na kumpatia matibabu, kwa kushirikiana na kituo kinachomlea, wameandaa chumba maalumu chenye umeme na mahitaji mengine muhimu kwa ajili yake.

Alitaja huduma ambazo MHN imempatia kuwa ni matibabu yote, gharama za kuwa hospitali kwa muda wote wa mwaka mmoja na miezi minne na kumpa mashine ya kumsaidia kupumua.

Pia, madaktari walioko kwenye mafunzo kwa njia ya vitendo, walichanga na kumnunulia mtungi wa oksijeni tiba.

Aligaesha alisema pia msamaria mwema mwingine amempa msaada wa mashine ndogo ya kupumulia.

"Sehemu ya vifaa hivi vitamsaidia wakati akiwa nje ya chumba chake, umeme ukikatika au akiwa na safari yoyote na wakati anakuja kuhudhuria kliniki au kufanyiwa vipimo kama mazoezi tiba," alifafanua.

Kuhusu gharama zilizotumiwa katika kipindi chote hadi kumuandalia makazi bora, Aligaesha alisema wamezihifadhi.

Aliwaomba wasamaria wema na watakaoguswa na kumsaidia kijana huyo, kutembelea kituo anachoishi Mikidadi kilichopo Kusarasini ili aweze kupata msaada kwa mahitaji mbalimbali.

Kwa upande wake, Mikidadi aliwashukuru madaktari, wauguzi na wote waliopigania uhai kipindi chote akiwa hospitali hapo.

Alisema aliishi hospitali hapo kama nyumbani na alipewa huduma zote tangu akiwa hawezi kupumua hadi sasa anaweza kupumua kwa kutumia mashine maalum.

Aliwasihi wasamaria wema wenye nia ya kumsaidia kufanya hivyo kwa sababu bado anahitaji msaada zaidi.

# 'Utafiti haujatumika mipango ya maendeleo'

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imesema pamoja na kutumia matokeo ya utafiti katika kutunga sera mbalimbali, lakini bado mchango wa utafiti katika mipango ya maendeleo nchini sio wa kuridhisha kutokana na matokeo mengi ya utafiti na taarifa za kitaalamu bado zinaishia kwenye majarida, makabati ya maktaba na ofisi.

Kauli hiyo ya serikali imetolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe, wakati akifungua mdahalo wa wazi wa uchambuzi wa matokeo ya utafiti katika utunzi wa sera na mipango ya maendeleo iliyofanyika katika Chuo cha Nelson Mandela Kampasi ya Solomon Mahlangu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) mkoani Morogoro.

Alisema serikali inategemea matokeo ya utafiti katika kufanya maamuzi na kusimamia maendeleo, hivyo imefika wakati sasa vyuo vikuu na taasisi zingine kuzalisha maarifa na ujuzi ili wazalishaji watumie matokeo hayo katika kuboresha na kuhusisha bidhaa na huduma kwa kuzitumia utafiti huo uliozalishwa na sio kuwekwa katika makabati na ofisi.

Alisema katika nchi zinazoendelea zinategemea sana uwekezaji katika utafiti za kisayansi, teknolojia, ubunifu na uvumbuzi, hivyo serikali kwa kuzingatia mahitaji na uhalisia wake imedhamilia sasa kujitolea kuwezesha taasisi mbalimbali na mtafiti mmoja mmoja kubuni na kuboresha sekta zote za kiuchumi ikiwamo sekta ya viwanda ambayo kwa sasa inakuwa kwa kasi kwa kutumia tafiti mbalimbali ili zitolewe kwenye makabati zisaidie kukuza uchumi.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Maulid Mwatawala, alisema sera na mipango ya kimaendeleo imekuwa ikipungukiwa urari licha ya kuwa na malengo makubwa kuliko uhalisia na mingine haiakisi mahitaji halisia ya jamii husika kutokana na tafiti na matokeo yake tafiti nchini hazitumiki ipasavyo na watunga sera na mipango ya maendeleo hawapati kirahisi na kwa lugha rafiki.

Alisema kutokana na muktadha huo, SUA imeona ni vyema kutumia uwezo wake wa ndani kwa kushirikiana na wadau wengine kuanzisha Kituo cha Usanisi wa matokeo ya utafiti ili kusanisi ushahidi wa utafiti katika uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo, kufanya mapitio ya machapisho ya kisayansi na kuandaa kanzidata ya matokeo mbalimbali ya utafiti na katika lugha rahisi pamoja na kuandaa mihutasari ya sera.

Mratibu wa Mradi wa kujenga na kukuza uwezo wa watafiti kusanisi matokeo ya utafiti ili ziweze kutumika katika maamuzi mbalimbali ya kisera kwa maendeleo ya nchi CREPEE, Dk. Faith Mabiki, alisema Afrika iko nyuma katika utoaji wa matokeo ya tafiti licha ya kuwa na idadi kubwa ya watu.

TANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

ISO 9001: 2015 IMETHIBITISHWA

# TAARIFA KWA UMMA

## MATUMIZI YASIYO SAHIHI YA NAMBA YA MLIPAKODI (TIN) ZISIZOHUISHWA NA ZISIZO ZA BIASHARA KATIKA UAGIZAJI WA BIDHAA KUTOKA NJE YA NCHI KWA AJILI YA UUZAJI HAPA NCHINI TANZANIA

**Dar es Salaam, 3 Septemba 2020:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania ("TRA" au "Mamlaka") inapenda kuufahamisha umma kuwa Mfumo Unganishi wa Uondoshaji Mizigo ya Forodha (TANCIS) umeboreshwa na kuweza kutambua Namba ya Mlipakodi (TIN) ambayo haijatumiki (iTIN) na/ama isiyo ya biashara (nTIN). Aidha, TRA hivi karibuni imebaini uwepo wa iTIN na nTIN zinazotumika na baadhi ya wafanyabiashara wasiowaaminifu kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi na kuziuza hapa nchini kinyume na matakwa ya Sheria kuhusu matumizi ya TIN. Hivyo basi, uboreshaji wa TANCIS, pamoja na mambo mengine, una lengo la kuiwezesha Mamlaka kupata taarifa sahihi za kikodi kwa wamiliki wa TIN ili kuhakikisha uhiari katika ulipaji kodi unafikiwa kwa kiwango cha juu kama ilivyo matakwa ya **Kifungu cha 5(1)(e) cha Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, SURA 399 R.E 2019.**

Kwa mujibu wa **Kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 R.E 2019,** TIN hutolewa kwa mtu ambaye anawajibika kulipa kodi kutokana na kufanya biashara au shughuli ya uwekezaji. Aidha, kwa mujibu wa **Kifungu cha 22(2)** cha Sheria hiyo, Kamishna Mkuu amepewa mamlaka ya kumtaka mtu yeyote kujisajili na kupata TIN kwa wakati wowote anaoweza kuamua kwa kadri atakavyoona inafaa. Kwa mantiki hiyo, na kutokana na nia njema ya uanzishwaji wa hivi karibu wa Mfumo wa Uwasilishaji Ritani kwa njia ya Kielektroniki ***(e-filing)***, na ambao unalazimu uwasilishaji wa taarifa muhimu za kikodi kwa njia ya mtandao, Kamishna Mkuu anaelekeza kwamba; Mosi, mtu yoyote mwenye lengo la kufanya shughuli inayohusiana na ulipaji kodi, kujisajili na kupata TIN ili kuiwezesha Mamlaka kubaini kodi sahihi kwa kila mhusika. Pili, wafanyabiashara na wawekezaji wanaotumia iTIN na nTIN waache mara moja.

Tafadhali tambua kwamba iTIN na nTIN zinatolewa kwa mujibu wa **Kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438, R.E 2019** kwa matumizi mahususi mathalani, upatikanaji wa Leseni ya Udereva au uagizaji magari kwa matumizi binafsi tu. Tunaomba ieleweke kuwa, wamiliki wa leseni za udereva ni waajiriwa katika Sekta ya Umma au Sekta Binafsi na magari waliyoagiza yanatumika kibiashara na kupata kipato, isipokuwa kama kuna ushahidi kuwa hayatumiki kibiashara. Hata kama magari husika hayatumiki kibiashara, ni ukweli kuwa wamiliki wa magari hayo ama walikuwa waajiriwa, au walifanya biashara au uwekezaji na kupata fedha walizotumia kununua magari hayo. Hivyo, TIN zao zilipaswa kuwa za kibiashara, kwa mujibu wa **Kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438, R.E 2019**, na wanalazimika kuleta taarifa za kikodi TRA ikiwemo ritani za kodi, isipokuwa wale waajiriwa ambao kodi zao zinalipwa na waajiri kwa utaratibu wa kodi ya zuio kupitia TIN zao.

Hivyo, kutumia mifumo yetu (ikiwemo TANCIS) kuanzia tarehe **1 Septemba 2020,** Mamlaka imeanza kufuatilia TIN zinazotumika kwenye matamko ya kiforodha **(customs declarations)** kujiridhisha endapo TIN hizo zinatumika kwa biashara au uwekezaji na mtu ambaye kwake TIN hiyo ilitolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 2 na **Kifungu cha 23(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 R.E 2019,** mtawalia. Hivyo, kufuatia zoezi hili la ufuatiliaji, Mamlaka inawaomba na kuwasihi walipakodi wetu kuhakikisha kwamba TIN wanazotumia kuondosha mizigo kwenye Himaya ya Forodha ni za matumizi ya ama biashara au uwekezaji kama ilivyo matakwa ya Sheria.

Ifahamike kwamba **Kifungu cha 91 cha Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332 R.E 2019,** kikisomwa pamoja na **Kifungu cha 46(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 R.E 2019**, iTIN na nTIN zinapaswa kutambulika kuwa ni za biashara na mhusika anapaswa kufaili ritani ya kodi ya mapato na kulipa kodi kutokana na biashara au uwekezaji anaofanya. Hivyo, ni vema wamiliki wa TIN hizo wakatumia fursa ya kufaili ritani zao kupitia mtandao (e-filing), utaratibu ambao umerahisisha uletaji wa ritani bila kufika Ofisi za TRA. Vinginevyo Kamishna Mkuu atawajibika kuwachukulia hatua kwa mujibu wa **Kifungu cha 78 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 R.E 2019** kwa kushindwa kuleta ritani hizo. Aidha, wamiliki wa TIN hizo watalazimika kuchukua hatua ya kuhakiki TIN zao ili ziweze kufutwa endapo Kamishna Mkuu ataridhia kuwa hawana kodi ya kulipa na hawastahili kuwa na TIN kwa mujibu wa Sheria. Iwapo mwenye iTIN na nTIN hatachukua hatua za makusudi kuhakikisha TIN yake inatumika kwa mujibu wa Sheria basi atakuwa anatenda kosa kwa mujibu wa **Kifungu cha 24 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 R.E 2019** na kwamba anaweza kutozwa faini kwa mujibu wa Sheria hiyo.

Ni wazi kuwa sehemu kubwa ya bidhaa zinazoingizwa nchini ni kwa ajili ya biashara. Hivyo, Mamlaka inatarajia kuwa faida zinazotokana na mauzo ya bidhaa hizo zionekane kwenye ritani za kodi ya mapato na si vinginevyo. Pia, ni matarajio yetu kuwa kwa wale ambao wanastahili kuandikishwa kwa ajili ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) wajisajili na kutimiza wajibu wao wa kukusanya kodi hiyo na kuiwasilisha TRA kupitia ritani zao za kila mwezi. Sambamba na hili, uangalizi wa TIN ulioanzishwa utazingatia uhakiki wa uingizaji wa bidhaa na mauzo ya ng'ambo yaliyofanyika kwa kutumia TIN zote zikilinganishwa na ritani za kodi zilizoletwa TRA ili kubaini wale wote ambao wanaingiza bidhaa nchini au kuuza ng'ambo lakini hawaleti ritani na kulipa kodi stahiki. Kwa kutumia **Kifungu cha 47 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 R.E 2019,** Mamlaka itawakadiria kodi wale wote ambao hawatatimiza wajibu wao wa kuleta ritani na kulipa kodi stahiki na watalazimika ama kulipa kodi hizo au kuzipinga kwa mujibu wa Sheria.

Ni rai ya Mamlaka kuwa walipakodi wote watumie TIN zao za biashara kwa usahihi wanapoagiza au kuuza bidhaa ng'ambo. Aidha, kwa kuwa tumeonesha kuwa wenye iTIN na nTIN ambazo zilitolewa kwa matumizi mahususi, kwa namna moja au nyingine walikuwa wanaendesha biashara au uwekezaji ambao kwao wangestahili kulipa kodi, hivyo, ama iTIN au nTIN ni TIN ya biashara na mhusika anawajibika kuleta ritani na kulipa kodi vinginevyo atakuwa hajatekeleza wajibu wake wa kisheria katika kutumia TIN.

Kwa maelezo zaidi, tutafurahi kuwasiliana na mtu yeyote kwa kutupigia simu ya bure **(toll free)** kupitia namba **0800750075 au 0800780078** au barua pepe **huduma@tra.go.tz**.

**Imetolewa na:**

**Dr. Edwin P. Mhede, Ph.D.**
**KAMISHNA MKUU**

215887702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *TFF, TPLB msifumbie macho viwanja vibovu*

**LIGI** Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21 ilianza rasmi jana kwa viwanja sita kuwaka moto nchini kabla ya kuendelea tena leo kukamilisha raundi ya kwanza kwa kupigwa katika viwanja vitatu.

Viwanja sita vilivyoshuhudiwa ligi hiyo, ikitimua vumbi ni Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya ambapo mabingwa watetezi, Simba walikuwa wageni wa Ihefu FC, huku dimba la Majaliwa mkoani Lindi Namungo ikiwa wenyeji wa Coastal Union ya Tanga.

Katika Uwanja wa CCM Gairo mkoani Morogoro, Mtibwa Sugar iliwaalika Ruvu Shooting, wakati Uwanja wa Jamhuri pale jijini Dodoma, wenyeji Dodoma Jiji waliwaalika Mwadui FC.

Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma, Biashara United ilikuwa wenyeji wa Gwambina FC huku mchezo wa mwisho kwa jana ukiwa ule wa usiku, Yanga ilipoikaribisha Tanzania Prisons ya Mbeya katika dimba la Mkapa.

Kwa ujumla msimu huu ambao unashirikisha timu 18 kutoka 20 za msimu uliopita, unaonekana ushindani utaongezeka zaidi, hasa kutokana na namna timu zilivyojipanga na zilivyoanza kwa kukamiana.

Tulishuhudia msimu uliopita, mbio za ubingwa zikimalizika mapema kwa Bingwa kujulikana, na vita ikahamia katika nafasi ya pili, lakini kubwa ilikuwa zinazopigana kujinusuru kushuka daraja.

Mwisho wa siku, Singida United, Ndanda FC na Mbao FC, ndizo zikaaga Ligi Kuu, huku Dodoma Jiji, Gwambina FC na Ihefu FC zikipanda na kuwa miongoni mwa timu 18 zinazowania ubingwa wa ligi hiyo msimu huu.

Hata hivyo, changamoto kubwa bado ni ubovu wa viwanja husuan eneo la kuchezea 'pitch', hivyo Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), hawana budi kulivalia njuga wakati ligi ikiendelea.

Wote tunafahamu ubovu wa viwanja nchini na jinsi ambavyo msimu uliopita vilikuwa vikilalamikiwa na makocha kuwa ni chanzo cha matokeo mabaya na wachezaji kupata majeraha, na kwa awali tu tayari tumebaini hali hiyo bado ipo na itaendelea kuziathiri timu.

Nipashe tumeshangazwa kuona sehemu kubwa ya viwanja vilivyotumika jana sehemu kubwa vikiwa na vipara vya nyasi, ukiacha ule wa Mkapa jijini Dar es Salaam na wa Kaitaba, Bukoba.


Tunajiuliza kama hali iko hivi ikiwa huu ndio mwanzo wa msimu, itakuwaje baada ya ligi kufikia angalau raundi ya tano ama sita? TPLB na TFF kwa hili wanaonekana wamelifumbia macho sana.

Nipashe tulianza kulipigia kelele mapema sana, lakini chakushangaza TPLB ikasubiri zikiwa zimesalia takriban wiki moja ndio ikaanza kutoa kauli.

Sisi tunatamani kuona hata ligi hiyo ikichezwa katika viwanja vitatu ama vinne tu ambavyo vina ubora kwa afya za wachezaji kuliko inavyochezwa viwanja takriban 10 kati ya hivyo sita vikiwa si rafiki.

Kama tunataka kuwa na ligi bora itakayovutia wawekezaji wengi nje na ndani ya nchi, ni lazima tuhakikishe kunakuwa na miundombinu rafiki kwa soka hasusan viwanja, hivyo TFF na TPLB hawana budi kulimulika zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# *Ligi imeanza, waamuzi waitendee haki*

**HATIMAYE** Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21 imeanza jana kwa mechi sita kucheza, huku zingine tatu zikitarajiwa kuendelea tena leo.

Hii ni baada ya kumalizika kwa Ligi Kuu msimu uliopita, ambayo pamoja na mambo mengine ilikuwa na baadhi ya matukio ya vibweka hasa kwa waamuzi.

Wengi wanakumbuka jinsi baadhi ya magoli ya kuotea kwa baadhi ya timu. Lakini mashabiki hawawezi kusahau moja ya mechi ambayo mwamuzi na mwamuzi msaidizi walishindwa kutafsiri sheria ya goli kwa kipa kudaka mpira kwenye mlingoti, ukiwa umezidi yadi kadhaa ndani ya nyavu.

Hata hivyo, badala ya kuwa bao, au siyo bao, waliamuru iwe kona na kuwa kituko cha mwaka, kiasi cha tukio lile kupachikwa jina la 'goli kona'.

Kifupi ni kwamba kwenye Ligi Kuu msimu uliopita, hakuna timu ambayo haikubebwa na waamuzi, lakini ambayo haikunyongwa na waamuzi.

Tuliona baada ya waamuzi kulalamikiwa sana na vyombo vya habari na mashabiki kiasi cha hata Shirikisho la Soka Nchini (TFF) na serikali kuingilia kati.

Kilichotokea ni kwamba, waamuzi walianza sasa kuchezesha kwa woga na kuanza kuzinyonga timu za Simba na Yanga ambazo kwa kiasi kikubwa ndizo zilizokuwa zikilalamikiwa kubebwa kwa baadhi ya mechi.

Sasa ilikuwa hata kama zikifunga magoli, kwa woga waamuzi wanakataa kwa madai wafungaji wameotea, lakini marudio ya picha za video yakionyesha kuwa haikuwa kweli.

Hayo tuyaache tuangalia msimu huu. Tayari Mwenyekiti wa Waamuzi, Sudi Abdi, ameahidi kuwa waamuzi watachezesha kufuata sheria zote na kanuni zake msimu huu.

"Tumewapa semina waamuzi wetu, tumewapima utimamu wa mwili, tumewafanyisha mazoezi uwanjani na darasani pia, tumewapima uelewa na pia tumewaangalia nyuma walifanya nini," alisema mwenyekiti huyo.

Akawahakikishia Watanzania kuwa makosa yatapungua kwa sababu na hata pale yatakapokuwa yanajitokeza, basi hawatosita kuyafanyia kazi.

Ni kweli kabisa, mashabiki wa soka nchini wanataka soka lichezeshwe kwa haki, ingawa kuna unafiki ndani yake, kwani hao hao wanaotaka hivyo, wanataka timu zao wanazozipenda zipendelewe na wasizozipenda kuminywe.

Na ukitaka uamini hilo ni kwamba mashabiki wa Simba hulalamika sana, inapoonekana kuna mechi Yanga inaonekana kama imebebwa, lakini mashabiki wa Yanga hivyo hivyo. Na mashabiki wa Simba na Yanga hao hao huwa hawalalamiki timu zao zinapobebwa, lakini huwa mbogo zinapoonekana kama zimeonewa.

Presha zao kwenye mitandao ya kijamii na kwenye vyombo vya habari zinakuwa kubwa mno.

Lakini zinapoonewa timu ndogo, inakuwa ni kama machozi ya samaki kubaki majini, labda usaidiwe na upande mmoja wa timu hizo mbili.

Sisemi kuwa waamuzi wachezeshe vizuri kwa asilimia 100 la hasha. Ulimwenguni kote hakuna waamuzi wa aina hiyo. Ndiyo maana hata baadhi ya Ligi Kuu Ulaya husaidia na teknolojia ya VAR, ambayo hata hivyo bado kuna mashabiki wanaona kama nayo inapendelea baadhi ya timu.

Mfano msimu uliopita, VAR ilionekana kama vile inaipendelea sana Liverpool, wakati sivyo. Huu ndiyo mpira na hili ndiyo soka.

Pamoja na hayo yote, waamuzi wana uwezo kabisa wa kuchezesha kwa kufuata sheria zote 17 na hata kama kuna makosa yakaonekana ni ya kibinadamu tu.

Tatizo la baadhi ya waamuzi wa Tanzania ni waoga wa kutoa maamuzi linapotokea tatizo au kosa, hapo ndipo matatizo yote yanapoanza, kwani baadaye ataanza kusawazisha mambo ili kuepuka lawama, lakini ndiyo kwanza anakuwa anazidi kuharibu.

Nitoe kila la heri kwa waamuzi wote nchini, na kuwaambia kuwa soka la Tanzania ili lisonge mbele, linategemea zaidi uchezeshaji wao mzuri, wa haki, usiokuwa na woga, kumpendelea au kumwonea mtu.

# 33,969 wajiandikisha shahada ya kwanza TCU ndani ya siku 6

**Na Romana Mallya**

WANAFUNZI 33,969 wamejiandikisha kuomba shahada ya kwanza katika vyuo mbalimbali ndani ya siku sita za maonyesho ya Elimu ya Juu, Sanyansi na Teknolojia.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Prof. Charles Kihampa, aliyasema hayo hayo jijini Dar es Salaam wakati tume ikifunga maonyesho hayo ya 15 aliyofunguliwa mwishoni mwa mwezi uliopita.

Prof. Kihampa alisema maonyesho hayo yamewezesha vijana kukutana na vyuo na kuomba nafasi za masomo ngazi mbalimbali katika dirisha la kwanza la uombaji linalotarajiwa kufungwa Septemba 25.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya washiriki wa maonyesho hayo, Mkurugenzi Mkuu wa Global Link Education, Abdulmalik Mollel, alisema bado zipo changamoto ndogo zinazozuia udahili kukua katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

"Katika jumuiya hii, tunaonekana tuna udahili mdogo kwa ngazi ya vyuo vikuu, ninashauri katika vyuo vikuu vya ndani vingango vya kumtambua au kumruhusu mwalimu apate ajira vijikite katika complicate base badala ya GPA kamba vyuo vya nje," alisema.

Aliomba utengeneze mfumo ili vyuo vikuu viweze kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi inayoendana na ya wahadhiri.

"Tunapoweka vigezo vya juu sana katika kumdahili mwalimu inawezekana tukajitengeneza ushindani mkubwa na uhitaji ya wale waliopo na vyuo kushindwa kupanuka kwa haraka," alisema.

Pia aliishukuru TCU kwa kuwasajili mawakala na kutoa amani kwao ya kufanya kazi vizuri.

Akijibu kuhusu changamoto huyo ya udahili mdogo, Mwenyekiti wa Bodi TCU, Prof. Mayunga Mkunya, alikiri kuwapo kwa changamoto hiyo na kueleza kuwa bado upo chini ikilinganishwa na nchi nyingine.

"Katika nchi za Afrika ambapo miaka miwili iliyopita udahili ulikuwa kama asilimia 8 kwa wale wanaokidhi vigezo, lakini sisi ni asilimia 4 tu, bado ipo chini sana na hatuna budi kuongeza bidii ili kupanua wigo wa udahili wa wanafunzi vyuo vikuu kwa kuzingatia ubora," alisema.

Prof. Mkunya alizitaka taasisi zote za elimu ya juu ziendelee kuunga mkono juhudi za serikali za kuongeza fursa za masomo kwa Watanzania bila kuathiri ubora.

Alisema kauli mbiu ya mwaka huu inayosema, 'Nafasi ya elimu ya juu katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo endelevu, imelenga kuzikumbusha taasisi zote kuwa zinawajibu wa kuleta mabadiliko chanja.'

Alisema serikali imeendelea kuhimiza taasisi za elimu kutoa elimu bora ili kuzalisha wabunifu, wenye uwezo wa kuhimili ushindani katika soko la kitaifa, kikanda na kimataifa.

Katika maadhimisho hayo TCU imewapatia vyeti washiriki vya kutambua ushiriki wao kwenye maonyesho hayo.



Meneja wa kituo cha Redio Planet Fm mkoani Morogoro, Doreen Mwinyi, akikabidhi msaada wa vifaa vya kujifunzia kwa mmoja wa watoto wanaolelewa katika kituo cha kulea watoto yatima cha Darul Muslmeen Manispaa ya Morogoro. **PICHA: FRANK KAUNDULA**

# Mkulima jela miaka 30, viboko 12 kwa kubaka

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi, imemuhukumu mkulima wa Kijiji cha Milola, Hamza Ahmadi Namtale maarufu kama Supu (25) kifungo cha miaka 30 jela na kuchapwa viboko 12, baada ya kupatikana na hatia ya kubaka mwanamke {55}.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi, Maria Batraine, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na pande zote.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hizo, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea na aliiomba Mahakama imuonee huruma kwa kutompa adhabu kali kwa kuwa ni mkosaji wa mara ya kwanza na alifanya hivyo kwa bahati mbaya.

Baada ya maelezo hayo, Mwanasheria wa Serikali, Emmanuel John, aliiomba Mahakama kumpa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine walio na tabia ya aina hiyo, kwa madai kitendo kilichofanywa na mshtakiwa hakiwezi kuachiwa hivi hivi bila kupatiwa adhabu kali.

John alisema kitendo cha mshtakiwa kumshambulia kwa kumpiga mlalamikaji kisha kumbaka ni unyama usiostaili kufumbiwa macho.

Hakimu alisema anafungwa kifungo cha miaka 30 jela na kuchapwa makalioni viboko 12.

Awali John, aliieleza Mahakama hiyo kuwa mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo Julai 15, mwaka huu, katika shamba eneo la Nanguka Bondeni, ambapo alimshabulia mlalamikaji kwa kumpiga kichwani na kuanguka chini.

John alidai baada ya mlalamikaji kuanguka chini, alimvua nguo zake ikiwamo ya ndani kisha kumwingilia, hali iliyomsababishia kupata maumivu makali mwilini, hivyo kupelekwa katika zahanati ya Milola kupatiwa matibabu.

## Tanzania yapiga vita unyanyapaa dhidi wagonjwa wa selimundo

**Na Mwandishi Wetu**

ASASI zinazojihusisha na ugonjwa wa selimundo (TANSCDA) kwa kushirikiana na serikali zinaendesha vita dhidi ya unyanyapaa wa ugonjwa huo nchini.

Mpango huo ulizinduliwa na serikali mjini Dodoma mwanzoni mwa mwezi huu na utadumu hadi mwishoni mwa Septemba ikiwa ni maadhimisho ya mwezi ya kuongeza uelewa juu ya ugonjwa huo ambayo hufanyika kila mwezi Septemba, duniani.

Akielezea juu ya vita hiyo, jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya TANSCDAzania, Dk. Deogratias Soka, alisema kaulimbiu ya mwaka huu katika maadhimisho hayo ambayo yalianzishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), ni "Ujue ugonjwa wa selimundo, ondoa unyanyapaa."

Ujumbe huo, alisema unalenga kuhimiza jamii kukomesha imani potofu kwa jamii zinazochochea matukio ya ubaguzi na hata kusababisha migogoro mbalimbali katika familia zenye watu wanaoishi na ugonjwa huo kama vile kuvunjika kwa ndoa.

"Watu wengi hawana uelewa sahihi wa ugonjwa huu kama vile imani kuwa wagonjwa hufa kabla ya kufikia umri wa miaka 18 na lawama dhidi ya wanawake kusababisha hali hiyo," alisema na kuongeza:

"Nataka nikuhakikishie mgonjwa wa siko seli akipatiwa huduma za kiafya ana uwezo wa kuishi sawa na watu wengine wasio na ugonjwa huo."

Alitoa mfano kuwa hapa nchini kuwapo kwa mgonjwa selimundo mwenye miaka zaidi ya 50 na duniani yupo mwenye ugonjwa huo mwenye miaka 90. Alisema kuzaliwa kwa mtoto anayeugua ugonjwa huo inatokana na wazazi wote wawili kuwa na vinasaba vya selimundo, ingawa wao hawaugui.

Alisema taarifa njema ni kuwa vipimo vya haraka vya kuchunguza vinasaba vya selimundo kwa kutumia damu vitaanza kupatikana hadi katika ngazi ya hospitali za wilaya nchini.

Mpango huo, alisema utaenda na uanzishaji wa kliniki za ugonjwa wa selimundo ambazo zitasaidia kutoa huduma na kuelimisha jamii.

Alisema tayari tathmini ya vipimo hivyo vya kisasa imefanyika na vikaonekana kuwa na ufanisi hivyo kwa sasa ni maaandalizi ya mipango ya usambazaji ambayo itaandamana na uelimishaji wa watoa huduma.

Alisema asilimia 6.7 ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano nchini husababishwa na ugonjwa wa selimundo na hiyo inachangiwa na kutokuwapo kwa vipimo vya kubaini ugonjwa huo mapema. Kutokana na hali hiyo alisema kupatikana kwa vipimo hivyo siyo tu kutazuia kutokea kwa vifo hivyo bali kutasaidia vijana wa kike na kiume kujua hali zao kabla ya kuzaa.

Alizitaja dalili za ugonjwa huo kuwa ni upungufu wa damu, maumivu makali, watoto kushindwa kukua vizuri, na wenye umri chini ya miaka miwili wanaweza kupata maumivu na kuvimba kwa vidole vya mikono na miguu.

Dalili zingine ni pamoja na homa za mara kwa mara, kuvimba kwa bandama, macho kuwa na rangi ya njano, maumivu ya kichwa na udhaifu wa mwili.

# Jafo ajinadi kufanikisha ujenzi zahanati, vituo afya

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Kisarawe, Selemani Jafo, amesema vituo vya afya vitatu na zahanati 13 zimejengwa katika jimbo hilo katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ambavyo vimeondoa changamoto ya huduma za afya iliyokuwa inawakabili wananchi wa maeneo ya vijijini.

Jafo alisema, kutokana na hali hiyo wananchi wanatakiwa kukumbuka na kuwapigia kura wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), waendelee kuongoza serikali kwa kipindi kingine cha miaka mitano kutekeleza miradi mikubwa zaidi.

Aliyasema hayo katika uzinduzi wa kampeni zake uliofanyika katika Kijiji cha Kwala, Kata ya Chole na kueleza miradi mikubwa iliyotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

"Kuna mambo tunajivunia Wanakisarawe yamefanyika katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, tuliahidi tumefanya ajenda ya vituo vya afya, zahanati na maji imefanikiwa kwa kiasi kikubwa, ninawaomba mchagueni Dk. John Magufuli kuwa rais, mimi nikawe mbunge wenu na madiwani wa (CCM), tukaendelee kuleta maendeleo," alisema Jafo.

Alisema, pamoja na kuboresha miundombinu ya elimu katika kipindi kilichopita, pia kwa awamu ijayo wilaya hiyo inatarajia kujenga shule za sekondari zaidi kuwaondolea adha wanafunzi kutembea umbali mrefu.

"Miaka mitano ijayo ajenda ya elimu tutaipa kipaumbele pale tulipoishia tutaendeleza lengo letu kuinua kiwango cha ufaulu, sasa Kisarawe imeanza kutangazika katika eneo la elimu tunataka iwe wilaya ya kuigwa katika mkoa wetu wa Pwani," alisisitiza.

Akizungumzia sekta ya kilimo, Jafo alisema, akipata ridhaa ya kuongoza jimbo hilo, atasimamia mikakati ya kilimo kiweze kutumika kama ajira na kuinua kipato cha wakazi wa wilaya hiyo.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano ijayo, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami utaendelea kutoka Kisarawe hado Maneromango.

Mgombea ubunge viti maalumu Mkoa wa Pwani, Subira Mgalu, alisema Wilaya ya Kisarawe inai vijiji 12 pekee ambavyo vimebaki kuunganishiwa nishati ya umeme.

Mgalu ambaye ni Naibu Waziri Nishati, alisema mwaka 2015, vijiji tisa kati ya 84 pekee vilikuwa na umeme na 72 ifikapo Septemba 30, vitakuwa vimekamilika kuunganishiwa nishati hiyo.

Katibu wa CCM Wilaya ya Kisarawe, Josephine Mwanga, aliwataka wagombea wa chama hicho pamoja na wanachama kufanya kampeni za kistaarabu kwa kuelezea sera za chama hicho.

# Wazazi mbaroni tuhuma kumwozesha mwanafunzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, limemtia mbaroni mama wa bibi harusi, Mirembe Jekeno na mjomba wa bwana harusi, Dula Mondea, kwa madai ya kumwozesha mwanafunzi wa kidato cha kwanza mwenye umri miaka 17 (jina limehifadhiwa).

Binti huyo alikuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Mwantini Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, na aliozeshwa kwa mahari ya Sh. milioni 1.5, binti na mume wake walitoroka kusikojulikana.

Tukio hilo lilitokea juzi katika Kijiji cha Jimonduli Kata ya Mwantini, baada ya maofisa maendeleo ya jamii wa halmashauri hiyo walioambatana na askari, kumtoa binti huyo ili aendelee na masomo.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Deus Mhoja, alisema ndoa ya mwanafunzi huyo ilifungwa usiku Septemba 3, mwaka huu.

Alisema mipango ya kuwozesha mwanafunzi huyo ilianza Desemba mwaka jana akiwa darasa la saba, na wazazi wake walishachukua mahari nusu, na baada ya kumaliziwa ndipo ikabidi ifungwe harusi, na kumkatisha masomo mwanafunzi huyo.

"Tunawashikilia wazazi wa pande zote mbili kwa kosa la kumwozesha na kumuoza mwanafunzi na kumkatisha masomo yake, kwa kukiuka sheria ya mtoto na elimu," alisema Mhoja na kuongeza:

"Pia watusaidie kumpata mtuhumiwa Samson Kulwa, ayekadiriwa kuwa na zaidi ya umri wa miaka 20, ambaye alitoroka na mwanafunzi baada ya kusikia anakuja kukamatwa, kwa kosa la kumuoa mwanafunzi na kuzima ndoto zake."

Mama mzazi wa mwanafunzi huyo, Jekeno, alikiri kumwozesha mtoto wake, kwa madai kuwa hapendi kusoma na hana uwezo darasani, ndio wakaamua kumtafutia mwanaume ili aolewe.

Kwa upande wake mjomba wa bwana harusi Mondea, baada ya kupewa adabu kidogo na askari Polisi, aliahidi kutoa ushirikiano wa kupatikana kwa mtuhumiwa (muoaji) pamoja na mwanafunzi huyo, kwa sababu ana jua mahali walipo.

Victoria Maro, Ofisa wa Dawati la Jinsia Polisi mkoani humo, ambaye alikuwapo eneo la tukio, alisema wamewakamata wazazi hao huku wakimsaka muoaji ambaye alitoroka na mwanafunzi, ili wachukuliwe hatua kali za kisheria na liwe fundisho kwa wengine.




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, akizungumza wakati wa mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusiana na mbio za NMB Bima Marathon zitakazofanyika Jumamosi ijayo. Kushoto ni mwakilishi wa waandaaji wa NMB Bima Marathon, Baraka Mtavangu na mwakilishi kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dk. Rehema Laiti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Muhongo ataja sababu JPM achaguliwe tena

**Na Gwamaka Alipipi,** MWANZA

ALIYEWAHI kuwa Waziri wa Nishati na Madini, Profesa Sospeter Muhongo, ametaja sababu tatu za mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, kuchaguliwa tena.

Profesa Muhongo ambaye kwa sasa anawania ubunge Jimbo la Musoma Vijijini, alisema Dk. Magufuli, anapaswa kuendelea kuwa rais kwa sababu amewezesha uchumi wa nchi kukua, pamoja na kupeleka nchi katika uchumi wa kati.

Akizungumza wakati wa mkutano wa kampeni za urais mjini Musoma juzi, Profesa Muhongo alisema Benki ya Dunia (WB), ilitaja Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati baada ya kuwa na pato la taifa la wastani wa mtu mmoja Dola za Marekani 1,080 sawa na Sh. 2,502,543.60.

Alisema mafanikio hayo yametokana na jitihada za Dk. Magufuli, hivyo anapaswa kupewa miaka mitano mingine ya uongozi ili kuiletea mafanikio zaidi taifa.

"Dk. Magufuli amefanikisha uchumi wa nchi kukua kutoka asilimia tano hadi saba, uchumi wa nchi yetu unakua kwa kasi kuliko ongezeko la watu, hivyo anafaa kuendelea kuwa rais kwa sababu analipeleka taifa sehemu nzuri," alisema Profesa Muhongo.

Alitaja sababu ya pili kuwa ni hatua ya Dk. Magufuli kuwezesha upatikanaji wa ajira husussani kwa vijana.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitano, idadi ya Watanzania waliopata ajira ni milioni sita na kwamba kwa miaka mitano mingine Dk. Magufuli amepanga kutengeneza ajira milioni nane.

"Ajira zimepatikana nyingi katika miradi ya maendeleo ambayo imetekelezwa na inayoendelea kutekelezwa, ninaamini zitaendelea kupatikana kulingana na ongezeko la uchumi." "Uchumi utafikia asilimia nane miaka mitano ijayo, ukitaka maendeleo ni lazima uhakikishe uchumi wa nchi yako unafikia asilimia nane, Dk. Magufuli nina imani atatufikisha huko."

Sababu nyingine aliitaja ni ustawi wa jamii, alisema taifa lolote lenye amani ni lazima liwe na ustawi katika jamii.

Alisema kuwa Dk. Magufuli katika kipindi cha mitano ya utawala wake amefanikisha upatikanaji wa huduma ya umeme mijini na vijijini, amefanikisha kupekeleka maji pamoja na ujenzi wa barabara.

"Anajenga bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere litakalokuwa na uwezo wa kuzalisha umeme zaidi ya megawati 2,100 na umeme huo utatosheleza mahitaji nchini pamoja na kuuza katika nchi za jirani. Naye Vedastus Mathayo, anayewania ubunge Jimbo la Musoma Mjini, alisema asilimia 95 ya wananchi wa Musoma Mjini wanakunywa maji salama na ifikapo mwishoni mwa mwaka huu takwimu itaongezeka hadi kufika asilimia mia.

"Dk. Magufuli tulikuomba ujenzi wa uwanja wa ndege katika Wilaya ya Musoma umetekeleza, hivi sasa mkandarasi yupo katika hatua za mwisho za kukamilisha maandalizi na kwamba Sh. bilioni 1.2 zimeshatumika kuwalipa fidia wakazi watakaopisha ujenzi."

# COSTECH yataja kikwazo kwa wabunifu

**Na Romana Mallya**

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), imesema miongoni mwa changamoto zinazowakabili wabunifu ni kuwa na ubunifu mzuri, lakini mwamko wa jamii kuzipokea ili kuzitumia bado ni mdogo.

Mkurugenzi Mkuu wa tume hiyo, Dk. Amos Nungu, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam katika maonyesho ya vyuo vikuu yanayoendelea viwanja vya Mnazi Mmoja ambako COSTECH imeyatumia kutoa elimu kwa washiriki kuhusu miongozo mbalimbali ya kutambua wabunifu na wagunduzi.

Dk. Nungu alisema kwa sasa kuna mwamko mkubwa wa vijana kuingia kwenye ubunifu na ugunduzi wa vitu mbalimbali kulingana na uhitaji kwenye jamii, lakini kutokana na changamoto ya upokelewaji tume huwajengea uwezo wa kuandaa vipeperushi vya kuwaongoza.

"Wengine unakuta kijana anakuja na wazo anaomba fedha, lakini ukweli ni kwamba unakuta wazo lake siyo la fedha ni la kumsaidia kivingine," alisema.

Alisema COSTECH tangu mwaka 2018 imekuwa ikiandaa miongozo mbalimbali.

"Mwaka 2018 tuliandaa mwongozo wa kuwatambua wabunifu na wagunduzi na mwaka huu 2020 tumeiandaa miongozo mingine ya kuratibu masuala ya utafiti Tanzania na kupitia maonyesho haya tunatoa elimu kwa washiriki ili kuwajengea uelewa," alisema.

Dk. Nungu alisema teknolojia na ubunifu ni suala mtambuka ambalo kila wakati hubadilika.

Kuhusu ubunifu unaoonyeshwa na vijana kutoka taasisi za vyuo vikuu, Dk. Nungu alisema unahamasisha wazazi na walezi kuona watoto wao siyo tu wanasoma bali pia wanabuni mambo mbalimbali kwa ajili ya Taifa.

"Dhana ya uchumi wa kati wa viwanda ndiyo hii lazima tuwawezeshe vijana wetu ili baadaye waweze kujiajiri," alisema.



Naibu Kamishna wa Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Msafiri Mbibo, akimpatia cheti mhitimu wa mafunzo kwa waajiriwa wapya Ally Zuma. Kulia ni Naibu Mkurugenzi Raslimali Watu na Utawala, Alice Lukindo na Kaimu Mkuu wa Chuo cha Kodi, Dk. Lewis Ishemoi, mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yajivunia chanjo kwa watoto asilimia 99

**Na Happy Severine,** MWANZA

SERIKALI imesema kiwango cha utoaji wa chanjo kwa watoto wachanga na wenye umri chini ya miaka mitano nchini kimeongezeka sana kutoka asilimia 94 mwaka 2014/15 kufikia kiwango cha asilimia 99 mwaka 2020.

Pia imebainika kuwa kiwango kilichobaki cha asilimia moja ni tatizo kwa watoto kwani wamekuwa hawapati chanjo kama inavyotakiwa na kusababisha kurudisha nyuma juhudi za serikali za kuwalinda watoto na magonjwa hatarishi dhidi yao.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkurugenzi wa Kinga Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leornald Subi, wakati akifungua mafunzo ya siku moja mkoani Mwanza kwa waandishi wa habari kutoka mikoa ya Mwanza, Simiyu, Shinyanga na Mara kuhusu chanjo.

Dk. Subi alisema mafanikio hayo ya kuongeza kwa kiwango cha utoleaji wa chanjo yametokana na serikali kuendelea kuboresha kitengo cha chanjo kwa kuongeza bajeti ya chanjo kutoka Sh. bilioni 10 mwaka 2014/15 hadi Sh. bilioni 30 mwaka 2020.

Alisema mbali na serikali kuongeza bajeti ya chanjo, maboresho makubwa yamefanyika kwenye maghala makubwa ya kuhifadhi chanjo, ambapo ukarabati wake umeghalimu zaidi ya Sh. bilioni 1.3 pamoja na kuboresha vyumba vya ubaridi ambavyo vimegharimu Sh. milioni 450.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa serikali imenunua magari ya kusambaza chanjo nchi nzima 74 yenye thamani ya Sh. bilioni 7.7, ambapo malengo ya maboresho hayo ni kuhakikisha kiwango cha utolewaji wa chanjo kwa watoto kinaongezeka na kuwa bora zaidi.

"Juhudi hizi zimesababisha baadhi ya magonjwa kutokomea kama polio, pepopunda kwa watoto wachanga, wodi za magonjwa ya surua kwa sasa hakuna, lakini magonjwa ya kuharisha nayo hakuna kwa sasa... haya magonjwa yalikuwapo zamani miaka 1999, lakini leo hakuna magonjwa haya," alisema Dk. Subi.

Meneja wa Mpango wa Taifa wa Chanjo, Dk. Dafrosa Lyimo, alisema magonjwa yanayoshughulikia kwa chanjo, yanasambaa kwa kasi kwenye jamii ambayo ina watu wengi ambao hawajapata chanjo na watu ambao hawapati chanjo wana nafasi kubwa zaidi ya kupata maambukizi ya magonjwa.

Alitoa wito kwa waandishi wa habari na wadau wengine kuhamasisha huduma za chanjo kuendelea kutolewa kama kawaida ili kuepuka milipuko inayoweza kutokea.

# Mpango wa mbolea bure waanza rasmi

**Na Mwandishi Wetu,** NZEGA

KAMPUNI ya mbolea ya YARA Tanzania imezindua mpango wa kuwasaidia wakulima wadogo kwa kuwapa mbolea bure unaolenga kuwafikia wakulima zaidi ya 83,000 katika kilimo cha mpunga na mahindi nchini.

Chini ya mpango huo, unaojulikana kama 'Action Africa', uzalishaji wa mazao ya mpunga na mahindi utaongezeka sambamba na kumhakikishia mkulima mdogo uhakika wa chakula na kuinua kipato cha familia kwa kuongeza uzalishaji.

Akizindua mpango huo wilayani Nzega, katika mkoani Tabora, Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Philemon Sengati, ameipongeza kampuni ya YARA kwa kuja na mpango huo utakaomhakikishia mkulima mdogo wa Kitanzania analima kilimo cha kisasa na bora kitakachomsaidia kujikwamua na kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa. "Mbolea tani 12,500 ya YaraMila Cereal yenye thamani ya shilingi bilioni 16.5 mliyoitenga kwa ajili ya kuwasaidia wakulima hapa nchini ikiwapo Tabora ni kubwa na itatoa mchango mkubwa katika sekta ya kilimo," alisema Dk. Sengati.

Alisema kampuni hiyo imekuwa mdau muhimu katika maendeleo ya sekta ya kilimo katika mkoa wake, hivyo atashirikiana bega kwa bega kuhakikisha mkulima mdogo na wakati ananufaika na kilimo ili kutoa mchango katika uchumi wa taifa.

Naye Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema serikali inaendelea kujenga mazingira rafiki kwa watoa huduma za kilimo ili waweze kufanya shughuli zao vizuri ikiwamo kutoa huduma za ugani, ushauri na kuwasimamia wakulima Tanzania nzima ili kuendelea kuiinua sekta ya kilimo nchini.

Alisema serikali imeshachukua hatua mbalimbali kuhakikisha sekta ya kilimo nchini inaanza kukopesheka kwa gharama nafuu kutoka asilimia 22 mpaka asilimia 13 na lengo ni kuona wakulima wa kitanzania wanapata mikopo mpaka chini ya asilimia 10 kwa kila shilingi.

"Tumedhamiria kuona sekta ya kilimo inakua na kutoa mchango stahiki kwa kuhakikisha mikopo inayotolewa katika sekta hii inakuwa na riba nafuu. Nawapongeza YARA kwa kufanya kazi karibu na wakulima," alisema Bashe.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mbolea ya YARA Tanzania, Winstone Odhiambo, alisema mpango huo unalenga kukuza uzalishaji wa mahindi na mpunga na kuihakikishia nchi inakuwa na chakula cha kutosha.

Veronica Shija, mkulima mdogo katika Kata ya Ijanija aliishukuru Kampuni ya YARA kwa namna ilivyo waunga mkono wakulima wadogo kwa kuwawezesha kupata mbolea bure na mbegu bora kwa gharama ya nusu bei.

## Wadau mawasiliano washauriwa utoaji taarifa mitandaoni

**Na Elizabeth Zaya**

MRATIBU wa Shirika lisilo la kiserikali la Paradigm Initiative Afrika nchini, Peter Mmbando, amewataka wadau wa mawasiliano kuzingatia utoaji wa taarifa zenye maudhui sahihi kwenye mitandao ya kijamii.

Mmbando alisema hayo wakati wa semina ya waandishi wa habari na watetezi wa haki za binadamu iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Katika semina hiyo, waandishi wa habari pamoja na watetezi hao wa haki za binadamu walijifunza namna nchi ya Nigeria na Kenya zinavyofanya kazi za utoaji na upashanaji wa habari.

Mmbando alisema lengo ni kuangalia namna ya kuwa na lugha moja ya utoaji wa taarifa mbalimbali ambazo hazina athari kwa jamii hususani za maendeleo kupitia vyombo vya habari na watetezi wa haki hizo za binadamu.

Mmbando pia alisema katika kipindi hiki cha uchaguzi ni vizuri watu wakawa na tahadhari kwa kuepuka kutoa taarifa ambazo ni za upotoshaji.

Pia aliwataka kufuata sheria na taratibu zilizowekwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika usambazaji wa taarifa zozote.

"Tutalinda haki za wananchi kupata habari lakini tunataka habari wanazozipata ziwe ni sahihi na siyo feki, unapodanganya jamii kwa picha, kwa video au kwa habari yoyote unaharibu na kukiuka taratibu za kisheria za mawasiliano," alisema Mmbando.

Kened Mmari, mshiriki katika semina hiyo, alisema kutokana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia duniani ni muhimu nchi zikaanza kuangalia sera na sheria mbalimbali zilizopo kwa kuhakikisha zinakuwa jumuishi ili zichagize maendeleo.

"Katika miaka ya hivi karibuni Tanzania tumetunga sheria nyingi zenye malengo mazuri, nyingine ni zile ambazo zinahakikisha tunakuwa na habari sahihi na za kweli mitandaoni pasipokuwa na habari za uongo na pia umewekwa usimamizi mzuri wa maudhui yanayowekwa mtandaoni," alisema Mmari.

"Kunapokuwa hakuna usimamizi wa kile kinachokwenda mtandaoni kuna hatari ya kuleta athari na hii tumeshuhudia katika nchi mbalimbali, kwa hiyo tunashukuru kwa jitihada hizi," aliongeza.

Mmari alisema pamoja na jitihada nzuri za kupambana na wapotoshaji mitandaoni, lakini alisema kuna haja ya serikali kuangalia upya viwango vya usajili wa mitandao ya kijamii na televisheni mtandao.

"Kuna changamoto ambazo zimewekwa na serikali za gharama kubwa ya usajili wa mitandao ya kijamii na televisheni mtandao, na kwa sababu hiyo vijana wengi wameshindwa kuzimudu na zinaathiri uwezo wao wa kujifunza na kuweka maudhui mtandaoni, kwa hiyo ni vema serikali ikaangalia upya jambo hili," alisema Mmari.

# UDSM, Empower zitakavyowainua wajasiriamali

**Na Sabato Kasika**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam, kimeingia katika ushirikiano wa miaka mitano na Kampuni ya Empower Limited ya jijini Dar es Salaam, na kusaidiana kutoa ujuzi kwa wanafunzi wa chuo hicho unahusiana na ujarisiamali na ubunifu.

Ushirikiano huo unaendana na ajenda ya mabadiliko ya uchumi wa Tanzania kwa kufanya uwekezaji kwa ajili ya kuwapa watu maarifa, ambao utawezesha taasisi za elimu, kampuni za kibiashara kushirikiana kuwapa uratibu mzuri na utekelezaji wa mpango wa kutoa ujuzi unaotakiwa katika karne ya 21. Akizungumza katika uzinduzi wa ushirikiano huo uitwao Generation Empower (GenEm), Naibu Makamu Mkuu chuo hicho (Utafiti), Prof. Bernadeta Killian, alisema, mpango huo wa miaka mitano utahusisha wanafunzi walio mwaka wa mwisho katika vitivo vyote.

"Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinafurahi kushirikiana na Empower kuleta mabadiliko chanya yanayowezesha kuwapatia ujuzi wa karne ya 21 wanafunzi 250 kila mwaka, sambamba na maarifa ya kusimamia vipaji vyao," alisema Prof. Killian.

Aliongeza kuwa hatua hiyo pia itawawezesha kuchangamana na wateja wa kampuni za kibiashara, ambapo alitoa wito kwa kampuni hizo kuunga mkono programu ya GenEm.

Mkurugenzi Mtendaji na mwasisi wa Empower Limited, Miranda Naiman, alisema, kazi ya kampuni hiyo kwa vijana wa Kitanzania ilianza miaka11 iliyopita.

"Tutafanya kazi kwa kuzingatia mipango ya kitaaluma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuwapa wanafunzi watakaofanikiwa kupitia katika programu hii ujuzi unaotakiwa kwa sasa," alisema Naiman. Alisema, lengo ni kuwapa wanafunzi hao maarifa zaidi ya taaluma zao na kuunganishwa katika fursa za ajira mara wanapohitimu, na kwamba kampuni zinaweza kufaidika na hao wenye ujuzi mkubwa na vipaji.

Mkurugenzi wa Ubunifu na Ujasiriamali wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Ambrose Itika, alisema chuo hicho kilianzisha kitengo cha ubunifu na ujasiriamali mwaka 2016.



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (kulia), akiteta jambo na Kaimu Mkuu wa Mauzo Vodacom Kanda ya Ziwa, Ahmed Akbarali na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, Suleiman Sekeite, wakati wa uzinduzi wa mpango wa kujenga kituo cha huduma kwa ajili ya wakulima kupitia programu ya M-Mkulima, wilayani Nzega. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi ushirika wanolewa kulima kilimo cha kisasa

**Na Mwandishi Wetu,**
SUMBAWANGA

VIONGOZI wa ushirika mkoani Rukwa wanapata mafunzo ili vyama vya msingi vya ushirika viweze kusimamia kwa ufanisi matumizi ya matrekta kama ilivyoainishwa katika mpango wa kuinua sekta ya kilimo awamu ya pili (ASDPII).

Mafunzo hayo yanatolewa kabla ya Kampuni ya Agricom Africa Company Limited kutoa matrekta kwa vyama vya msingi vya ushirika, ili kuinua uzalishaji wa mahindi katika kila wilaya ya mkoa wa Mpanda.

Kwa mujibu wa programu hiyo, chama cha msingi chenye wanachama wanaozidi 72 ambacho kitakuwa na fedha ya awali ya kulipia matrekta kitapewa matrekta ili kuinua uzalishaji wa mazao na kuinua kipato cha wakulima kama ASDP II inavyotaka.

Akizindua mafunzo hayo, Katibu Tawala Msaidizi (Uchumi na Uzalishaji), Ocram Chengula, ameisifu kampuni ya Agricom Africa kwamba inatekeleza kwa vitendo programu ya ASDP II. "ASDP II imejielekeza katika kuhakikisha matumizi ya zana bora za kilimo zinawafikia wakulima nchini ili kuongeza tija ya uzalishaji mazao nchini. Kampuni hii ASDP II kwa vitendo," amesema Chengula.

Alisema asilimia kubwa ya wakulima wa Rukwa wanatumia jembe, wanyama kazi na wachache wanatumia matrekta na kuongeza kwamba mafunzo hayo yatakuwa chachu ya kuanza kutumia zana za kisasa katika kuinua kilimo biashara, na kuongeza kwamba uzinduzi wa programu hiyo utaongeza hamasa ya uzalishaji wa mazao hususani mahindi na kuufanya mkoa kutosheleze kwa chakula.

Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Agricom Africa, Remmy Nindi, alisema kampuni yake inaelewa mkoa wa Rukwa una fursa kubwa za uzalishaji wa mazao ya mahindi.

"Rukwa ina nafasi kubwa ya uzalishaji kwa wingi zao la mahindi kutokana na ardhi yake. Hivyo kwa kuwapatia elimu ya matumizi ya zana za kisasa za kilimo kutaongeza uzalishaji mara tatu ya walivyokuwa wakizalisha awali," alisema Nindi. Amesema kampuni yao ina matawi Morogoro, Mbeya, Dodoma na Kahama.

Nipashe
Spotika




WANAMICHEZO 10 WANAOLIPWA ZAIDI DUNIANI UK. 12&13




SUAREZ

## ISIKUPITE

Mason Greenwood atavaa jezi namba 11 katika klabu ya Manchester United msimu huu 2020-21, lakini namba saba bado haina mtu.




# NYOTA WA4 WANAOWEZA KUTEMWA BARCA

**BARCELONA,** Hispania

RONALD Koeman amechaguliwa kuwa mrithi wa Quique Setien pale Barcelona.

Raia huyo wa Uholanzi ataangalia uwezekano wa kuwaachia wachezaji kadhaa waondoke wakati wa kipindi hiki cha majira ya joto, ili kupata nafasi ya damu changa.

Msimu wa 2019-20 umethibitisha kwamba, Barcelona inahitaji mabadiliko makubwa baada ya kumaliza bila taji lolote kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2013-14.

Wakiwa wameanza msimu na Ernesto Valverde kama kocha wao, Barcelona waliamua kuachana na Mhispania huyo katikati ya msimu baada ya kocha huyo wa zamani wa Athletic Bilbao kushindwa kupata matokeo mazuri.

Quique Setien aliteuliwa kama mrithi wake, lakini mambo yalishindwa kwenda sawa na akafukuzwa. Barcelona waliachia taji la ligi kwa wapinzani wao Real Madrid na pia walitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kichapo cha fedheha cha mabao 8-2 na Bayern Munich.

Koeman sasa amepewa jukumu la kujenga upya Barcelona na mlinzi huyo wa zamani wa klabu hiyo ya Katalunya kwa vyovyote ataanza kwa kuwafyeka wachezaji wanaoonekana umri kuwatupa mkono. Hawa ni wachezaji wanaoweza kukutana na panga hilo;

### #4 ARTURO VIDAL

Arturo Vidal sasa ubora wake unaonekana kufikia mwisho na kuna uwezekano mkubwa akaachiwa kuondoka hapo Barcelona ili kutoa nafasi kwa wachezaji vijana.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 33 anayetumia sana nguvu alikuwa msaada kwa Barcelona tangu alipotua hapo akitokea Bayern Munich mwaka 2018, lakini sasa kiwango chake kinaonekana kuporomoka.

Vidal raia wa Chile sasa ana uwezekano mkubwa wa kuondoka kipindi cha majira ya joto na anatajwa kwamba anaweza kwenda Inter Milan, ambako anaweza kwenda kuungana na kocha wake wa zamani Antonio Conte.

### #3 SERGIO BUSQUETS

Sergio Busquets ni kiungo wa tatu kwenye orodha hii ambaye naye anahitaji kukaa pembeni ili kupisha damu changa.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 32 na kwa namna yoyote ujio wa Miralem Pjanic ambaye amejiunga na timu hiyo kipindi cha majira ya joto kutoka Juventus, kutamfanya kuangalia njia ya kutokea.

Akiwa amefanya kazi na Frenkie de Jong kwenye timu ya taifa ya Uholanzi, Koeman ana uhakika wa kumtumia kijana huyo wa Kiholanzi kama ndio nguzo yake kwenye safu ya kiungo. Pamoja na Pjanic na uwepo wa Puig, Alena, na Sergi Roberto, safari ya Busquets ipo tayari.

### #2 SAMUEL UMTITI

Ndoto ya Samuel Umtiti kutamba hapo Barcelona sasa inaonekana ni kama imeyeyuka. Mfaransa huyo alijikuta hayupo kwenye kikosi hicho kutokana na mara nyingi kusumbuliwa na majeruhi, huku Clement Lenglet akitumika kama ndio patina wa Gerard Pique kwenye safu ya ulinzi.

Rekodi za hivi karibuni za Umtiti kwa namna yoyote zinamfanya achiwe kuondoka, huku nyota wa Manchester City, Eric Garcia akiwa amewashiwa taa ya kijani kurudi Barcelona.

### #1 LUIS SUAREZ

Ili kujijenga upya, Barcelona imeshafanya maamuzi magumu kadhaa. Na sasa wapo kwenye nafasi ya kufanya maamuzi mengine magumu ya kuachana na Luis Suarez kipindi hiki cha majira ya joto, akiwa anaingia kwenye mwaka wake wa mwisho katika mkataba wake.

Nyota huyo wa kimataifa wa Uruguay ni mmoja wa washambuliaji bora zaidi katika historia ya hivi karibuni ya klabu hiyo, akiwa ameshinda mataji 13 tangu ajiunge nao kutoka Liverpool kipindi cha majira ya joto mwaka 2014. Hata hivyo, misimu ya hivi karibuni imekuwa migumu kwa Suarez.

Barcelona wanaweza kuangalia uwezekano wa kumwachia kipindi hiki cha majira ya joto, huku Ajax ikionyesha nia ya kutaka kumsajili.

Klabu hiyo ya Katalunya sasa itatazamia kumtumia zaidi Antoine Griezmann kama mshambuliaji wao namba moja, huku pia wakihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili straika wa Inter Milan, Lautaro Martinez.

Suarez anaonekana hawezi kuwa kwenye mipango ya muda mrefu ya Barcelona na anaweza kuwa mmoja wa wachezaji wakubwa ambao wataondoka klabuni hapo kipindi cha majira ya joto.

## Extra Time



FEDERER

# WANAMICHEZO 10 WANAOLIPWA ZAIDI DUNIANI MWAKA HUU

**LONDON,** England

KUMEKUWA na kushuka kwa kipato kwa wanamichezo wengi duniani kutokana na hali ya mlipuko wa virusi vya corona ilivyo hivi sasa. Wakati nyota wa mpira wa mguu kama Cristiano Ronaldo na Lionel Messi wakiwa wameathirika zaidi, wanamichezo wengine pia wamekumbwa na athari hiyo kwa sababu ya hali ilivyo hivi sasa.

**Hata hivyo, wanamichezo maarufu hawategemei tu mishahara kukuza kipato chao. Kampuni kubwa zimekuwa zikiingia mikataba kwa ajili ya kutangaza bidhaa zao, matokeo yao wanajikuta wakiingiza mkwanja mrefu kwa miaka mingi.**

Wakati mpira wa kikapu na soka ikiwa ndio maarufu zaidi duniani, wanamichezo kama Tiger Woods na Roger Federer wameonyesha upekee wao.

Hapa tunawaangalia wanamichezo 10 wanaolipwa zaidi duniani mwaka huu:

### #10 CARSON WENTZ- DOLA MIL 59.1

Ni mchezaji wa soka la Marekani, Carson Wentz anashika nafasi ya 10 kwenye orodha hii duniani.

Nyota huyu mwenye umri wa miaka 27 anaingiza kiasi cha dola milioni 4 kutoka katika kampuni mbalimbali ambazo anatangaza bidhaa zake na anachukua mshahara wa dola milioni 55 pamoja na bonasi.

### #9 KIRK COUSINS- DOLA MIL 60.5

Huyu pia ni mchezaji wa soka la Marekani, Kirk Cousins alisaini mkataba wa dola milioni 84 akiwa mchezaji huru na kutua Minnesota Vikings mwaka 2018, ambapo wakati huo ilimfanya kuwa mchezaji anayelipwa zaidi katika historia ya Ligi Kuu ya soka ya Marekaani, NFL.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 32 pia ametengeneza jina lake katika timu ya Washington Redskins kabla ya kuhamia Minnesota Vikings, ambaye hivi karibuni alisaini mkataba wenye thamani ya dola milioni 66.

Cousins anaingiza dola milioni 2.5 kutokana na matangazo na pia anachukua dola milioni 58 kama mshahara wake na bonasi.

### #8 TIGER WOODS- DOLA MIL 62.3

Mmoja wa wanamichezo maarufu katika kizazi cha sasa, Tiger Woods anachukuliwa kama ndio mchezaji gofu bora zaidi wa wakati wote.

Alitawala mchezo huo kuanzia miaka ya 2000, Woods alishinda mataji makubwa 13 katika mashindano yote kutoka mwaka 1999 hadi 2010. Wakati wa kipindi chake, alikuwa mchezaji bora wa gofu kuanzia Agosti mwaka 1999 hadi Septemba 2004, na halafu Juni 2005 hadi Oktoba 2010.

Majeruhi yalimwandama na kusababisha kushuka kwa kiwango chake, lakini Woods mwenye umri wa miaka 44 alirudi akiwa imara na kushinda taji la Masters mwaka 2019. Analipwa euro milioni 60 kutokana na matangazo na dola milioni 2.3 kutoka kwenye mshahara wake pomoja na bonasi.

### #7 KEVIN DURANT- DOLA MIL 63.9

Aliukosa msimu wote wa 2019-20 kutokana na kuumia kisigino cha mguu, lakini Kevin Durant amebakia kuwa mmoja wa wachezaji maarufu zaidi wa mpira wa kikapu katika kizazi cha sasa.

Durant alijiunga na Brooklyn Nets kutoka Golden State Warriors mwaka 2019, akisaini mkataba wa miaka minne mwenye thamani ya dola milioni 164.

Anaingiza dola milioni 35 kutokana na mikataba ya makampuni tofauti, na anachukua nyumbani dola milioni 28.9 kama mshahara wake na bonasi.

### #6 STEPHEN CURRY- DOLA MIL 74.4

Anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji wa mpira wa kikapu bora zaidi katika kizazi chake, Stephen Curry.

Alitajwa mara mbili kama mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi kwenye Ligi Kuu ya Kikapu ya Marekani, NBA, na ameshinda mara tatu ubingwa wa NBA akiwa na Golden State Warriors.

Mkali huyo mwenye umri wa miaka 32 analipwa dola milioni 44 kutokana na matangazo binafsi na dola milioni 30.4 kama mshahara wake pamoja na bonasi.

#5 LeBRON JAMES- Dola Mil 88.2

Mara kwa mara anasifiwa na wengi kama ndio mchezaji bora wa kikapu wa wakati wote, LeBron James ni wa tatu na wa mwisho katika orodha hii kwa wachezaji wa mpira wa kikapu.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 35 kwa sasa anakiwasha katika timu ya Los Angeles Lakers, awali akiwa amecheza katika timu za Cleveland Cavaliers (mara mbili) na Miami Heat.

James anachukua nyumbani dola milioni 60 kutokana na matangazo na kwenye mshahara wake analipwa dola milioni 28.2 pamoja na bonasi.

### #4 NEYMAR JR. – DOLA MIL 95.5

Mmoja wa sura zinazotambulika zaidi duniani kwa sasa, Neymar ni mmoja wa wachezaji bora wa soka duniani.

Akiwa ameanza kucheza soka kule Santos, Neymar alitua barani Ulaya mwaka 2013 wakati alipojiunga na Barcelona na kufurahia mafanikio kwa kutengeneza upatina mzuri wa safu ya ushambuliaji pamoja na Lionel Messi na Luis Suarez. Alihamia Paris Saint-Germain kwa euro milioni 222 mwaka 2017, ada iliyoweka rekodi ya dunia.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Brazil ni mmoja wa wachezaji muhimu kwa miamba hiyo ya Parisien, na alikuwa mchezaji muhimu wakati wakitinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita. Anaingiza dola milioni 25 kutokana na matangazo na mshahara wake ni dola milioni 70.5 pamoja na bonasi.

### #3 LIONEL MESSI- DOLA MIL 104

Bilasha ni mchezaji bora wa wakati wote kwenye soka, Lionel Messi.

Akiwa ni muhitimu wa kituo cha kulelea vipaji cha La Masia, na akaja kuwa nembo ya Barcelona. Licha ya Barcelona kuwa na matokeo mabaya msimu uliopita, Messi alikuwa mpigaji pasi bora na mtengezaji mabao bora.

Iliripotiwa kwamba, Messi ameomba kuondoka Barcelona kipindi hiki cha majira ya joto baada ya kuchezea kichapo cha mabao 8-2 kutoka Bayern Munich kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kabla ya kubadili uamuzi wake. Anaingiza dola milioni 32 kutokana na matangazo binafsi na mshahara wake ni dola milioni 72 pamoja na bonasi.

### #2 CRISTIANO RONALDO- DOLA MIL 105

Mchezaji ambaye analeta ushindani mkubwa kwa Lionel Messi ni Cristiano Ronaldo.

Kama ilivyo kwa Messi, wengi wanabainisha kwamba Cristiano Ronaldo ni mchezaji bora wa wakati wote akiwa amefurahia mafanikio nchini England, Hispania na sasa Italia. Yeye ni mfungaji wa wakati wote wa Real Madrid, na katika umri wa miaka 35, ameendelea kucheza kwa kiwango cha juu kabisa kule Juventus.

Raia huyu wa Ureno ambaye alishinda taji la Euro mwaka 2016, anaingiza dola milioni 45 kutokana na matangazo binafsi na mshahara wake ni dola milioni 60 pamoja na bonasi.

### #1 ROGER FEDERER- DOLA MIL 106.3

Anatajwa kama ndio mchezaji bora wa tenis wa wakati wote, Roger Federer na ndio anashika nafasi ya kwanza katika orodha ya wanamichezo wanaolipwa zaidi duniani.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 39 ameendelea kuwa imara kwenye mchezo huo kwa kuonyesha kiwango cha juu. Federer ameshinda mara 20 taji la Grand Slam, ndio bora zaidi katika historia kwa mchezaji wa kiume.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswisi anaingia dola milioni 100 kutokana na matangazo yake binafsi na mshahara wake ni dola milioni 6.3 pamoja na bonasi.

## Nukuu

"Alikuwa na mchango mkubwa kwenye maamuzi yangu ya kuja hapa Chelsea hasa kwa sababu nilikuwa napenda kumwangalia jinsi alivyokuwa akicheza," **amesema Kai Havertz akimzungumzia kocha mkuu wa Chelsea, Frank Lampard.**




"Dani alikuwa sehemu ya kikosi chetu kilichofanya vizuri msimu uliopita na alikuwa na kiwango cha kuvutia. Napenda hamasa ya Dani na ni mchezaji mwenye uwezo wa juu," **amesema kocha Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta akimzungumzia Dani Ceballos ambaye amesajiliwa tena kwa mkopo kuichezea klabu hiyo.**



"Mpango wa mchezo wetu hautabadilika dhidi ya Uholanzi, lakini tutabadilisha wachezaji," **amesema kocha wa timu ya taifa ya Italia, Roberto Mancini akizungumzia mchezo wake dhidi ya Uholanzi kwenye michuano ya Ligi ya Mataifa ya UEFA utakaopigwa leo Jumatatu.**





# VIWANJA VITAKAVYOTIMUA VUMBI LIGI KUU 2020/21

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara ilianza jana kwenye mechi sita kupigwa kwenye viwanja mbalimbali nchini Tanzania. Ni safari ndefu ya kumsaka bingwa mpya wa msimu huu, huku timu 18 zikishikana mashati kuusaka kwa udi na uvumba.

**Timu zote 18 zitacheza mechi mbili kwenye viwanja vya nyumbani na ugenini. Timu hizo ni Simba, Yanga, Azam, Polisi Tanzania, Coastal Union, Biashara United, Dodoma Jiji, Gwambina FC, JKT Tanzania, KMC, Kagera Sugar, Mbeya City, Mtibwa Sugar, Mwadui FC, Namungo, Ruvu Shooting na Prisons.**

Kwenye makala haya tutaviangalia viwanja vitakavyokwenda kutumika kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

**1. UWANJA WA BENJAMIN MKAPA**

Ndiyo uwanja mkuu nchini Tanzania uliopo Dar es Salaam. Siyo kwa jina tu, bali hata ukubwa, lakini ubora wa uwanja wenyewe. Ni uwanja ambao hutumiwa zaidi na timu za Simba na Yanga kama uwanja wao wa nyumbani.

Mara nyingi, pamoja na ubora wake, lakini timu nyingi za mikoani hupata tabu sana zinapocheza na timu hizo mbili kutokana na ukubwa wa eneo la kuchezea, lakini wingi na mashabiki wa timu hizo uwanjani.

**2. UWANJA WA UHURU**

Huu ni uwanja mkongwe zaidi nchini Tanzania. Ndiyo ambao nchi ilipopatia Uhuru, bendera ya Mwingereza iliposhushwa na kupandishwa ya Tanganyika wakati huo, sasa Tanzania.

Nao pia utatumika kwa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara. Hutumika kama uwanja wa nyumbani kwa timu za Simba na Yanga kwa baadhi ya mechi, hasa ule ya Mkapa unapokuwa umefungwa kwa matengenezo, au kupumzishwa. Lakini uwanja huu hutumiwa na timu zilizopo Dar es Salaam, kama vile KMC kama uwanja wa nyumbani.

**3. UWANJA WA MABATINI**

Uwanja huu uliopo Mlandizi mkoani Pwani, unatumiwa na timu ya Ruvu Shooting kama uwanja wake nyumbani. Ni moja kati ya viwanja vinavyotumiwa kwenye Ligi Kuu kwa muda mrefu sasa.

**4. UWANJA WA JAMHURI MOROGORO**

Ni moja kati ya viwanja vya muda mrefu kuchezewa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara. Uwanja huu hutumiwa na Mtibwa Sugar kama uwanja wake wa nyumbani, hasa inapocheza na timu mbili kubwa zenye mashabiki wengi, Simba na Yanga.

**5. UWANJA WA CCM GAIRO**

Mtibwa Sugar, tangu msimu uliopita imekuwa ikiutumia uwanja huu kama uwanja wake wa nyumbani. Na msimu huu pia itaendelea kuutumia uwanja huo kwa mechi nyingi, ukiondoa za Simba na Yanga.

**6. UWANJA WA JAMHURI DODOMA**

Msimu huu utatumiwa na timu mbili. Timu ya Dodoma Jiji ambayo imepanda Ligi Kuu itautumia, lakini tangu msimu uliopita, timu ya JKT Tanzania iliutumia kama uwanja wa nyumbani na msimu huu pia itaendelea kuwa hivyo, kwa maafande hao wamehamia Dodoma.

**7. UWANJA WA SOKOINE**

Timu za Mbeya City na Ihefu FC zitautumia uwanja huu kama uwanja wao wa nyumbani uliopo Mbeya.

Hata hivyo, inawezekana kabisa Ihefu, ikautumia kwenye mechi mbili za Simba na Yanga.

**8. UWANJA WA HIGHLAND ESTATE**

Ni uwanja unaomilikiwa na klabu ya Ihefu FC. Upo maeneo ya Mbarali Mbeya na hivi sasa upo kwenye matengenezo, hivyo mechi za timu hiyo zinachezwa hapo ukikamilika, isipokuwa mechi dhidi ya Simba na Yanga.

**9. UWANJA WA GWAMBINA**

Gwambina FC, inayocheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu huu baada ya kupanda, inamiliki uwanja wake wenyewe uliopo maeneo ya Misungwi mkoani Mwanza. Yenyewe itacheza mechi zote za nyumbani kwenye uwanja wake.

**10. UWANJA WA MKWAKWANI**

Uwanja huu mkongwe kabisa nchini, kama kawaida, utakuwa na jukumu la kuihodhi timu ya Coastal Union, huko mjini Tanga.

**11. UWANJA WA KAITABA**

Kagera Sugar, huutumia uwanja huu wenye nyasi bandia kama uwanja wake wa nyumbani, hivyo nao uko kwenye orodha ya viwanja vitakavyotumika.

**12. UWANJA WA KAMBARAGE**

Ni uwanja unaotumiwa na timu ya Mwadui kwa mechi kubwa mbili tu, ikicheza na Simba au Yanga huko mjini Shinyanga.

**13. UWANJA WA MWADUI COMPLEX**

Unamilikiwa na timu ya Mwadui, na hutumika na Mwadui FC, inapocheza mechi zingine mjini Shinyanga, isipokuwa Simba na Yanga tu.

**14. UWANJA WA AZAM COMPLEX**

Uwanja huu uliopo Chamazi jijini Dar es Salaam, unamilikiwa na klabu ya Azam FC, na huutumia kama uwanja wake wa nyumbani. Ni mmoja kati ya viwanja viwili tu nchini, na Mkapa ambacho mechi zinaweza kuchezwa usiku kwa sababu vita taa.

**15. UWANJA WA NELSON MANDELA**

Uwanja huu uko Sumbawanga mkoani Rukwa. Mkoa huo hauna timu ya Ligi Kuu, lakini timu ya Prisons ya Mbeya, imeamua kwenda huko na kuufanya msimu huu kuwa uwanja wake wa nyumbani.

**JE, WAJUA?**



Mchezaji mpya wa Chelsea, Timo Werner, mwenye umri wa miaka 24 raia wa Ujerumani, alikataa nafasi ya kuhamia Manchester City baada ya kocha, Pep Guardiola kumpigia simu na kuzungumza naye ili amsajili.





# Mapato ya ndani kutekeleza miradi kimkakati ya bil. 215/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, ametaja miradi ya kimkakati 14 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 215 inayotekelezwa na inayotarajiwa kutekelezwa kupitia mapato ya ndani ili kuongeza mapato, kutoa huduma kwa wananchi na kupendezesha mji.

Mafuru aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na gazeti hili juu ya mikakati ya Jiji hilo kujiimarisha kimapato na mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka mitano (2014/15 hadi 2019/20).

Alisema kwa sasa Jiji hilo linajenga mradi wa 'Government City Complex' katika Mji wa Serikali Mtumba kwenye eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 35,152.4.

"Mradi huu una thamani ya Sh.bilioni 59.31 ambapo kwa sasa ujenzi upo awamu ya kwanza kwa gharama ya Sh. bilioni 18.87 na Sh. bilioni 4.1 zimelipwa," alisema.

Aidha, alisema kuna mradi wa ujenzi wa hoteli (Dodoma City Hotel) inayojengwa katikati ya mji kwenye eneo maarufu la 'Paradise cinema hall' ambao una thamani ya Sh. bilioni 9.99 ambazo zinatokana na mapato ya ndani ambapo hadi sasa Sh. bilioni 3.44 imetumika.

Kadhalika, alisema Jiji hilo lina mpango wa kutekeleza miradi mingine mikubwa ya kimkakati ambayo tayari imeshasanifiwa ikiwamo mradi wa Nunge wenye thamani ya Sh. bilioni 5.74.

Alitaja mingine ni City Complex Apartment yenye thamani ya Sh. bilioni 20.85, N.K Complex yenye thamani ya Sh. bilioni 31.77, City Complex Mall yenye thamani ya Sh. bilioni 62.17 na Nyerere Square Plaza yenye thamani ya Sh. bilioni 27.

"Pia ujenzi wa mradi wa maji Njedengwa wenye gharama ya Sh. bilioni 1.4, ujenzi wa mradi wa maji Hombolo wenye Sh. milioni 610, ujenzi wa mradi wa maji Chihikwi wenye gharama ya Sh. milioni 90.6," alisema.

Mafuru alisema pia halmashauri imefanikiwa kuandaa miongozo ya uwekezaji kwa ajili ya kuongoza utekelezaji wa miradi.

"Jiji limetekeleza ujenzi wa miradi ya vituo vya afya Makole, Mkonze, Hombolo, pia limefanikiwa ujenzi wa masoko ya Kikuyu, Chadulu na Bonanza, pia kuboresha minada ya Mpunguzi na Msalato," alisema.

Pamoja na hayo, mkurugenzi huyo alisema kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2019/20 imetolewa mikopo ya Sh. bilioni 5.29 kwa vikundi 1,259.



Umoja wa vijana wa soko la Sabasaba wakishirikiana kufanya usafi wa mazingira na watoto wenye mahitaji maalum wa kituo cha Cheshira kilichopo Miyuji jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mavunde aahidi kuing'arisha Dodoma kimaendeleo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MGOMBEA wa ubunge Jimbo la Dodoma Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Anthony Mavunde, amezindua kampeni zake, huku akiwaahidi kuing'arisha Dodoma kimaendeleo kwenye nyanja mbalimbali.

Akizungumza na wakazi wa jimbo hilo, kwenye viwanja vya shule ya msingi Chang'ombe, Mavunde alisema miaka mitano ya kwanza ambayo wananchi wameshuhudia Dodoma ikikua kwa kasi ilikuwa ya yeye kujifunza, lakini wakimchagua tena watashuhudia makubwa kwenye sekta ya afya, elimu, maji, miundombinu na michezo.

Alibainisha kuwa katika sekta ya elimu atahakikisha wanafunzi wanasoma kisasa na atatoa kompyuta kwa shule zote za msingi na sekondari kwenye jimbo hilo.

"Katika ubunge wangu wa miaka mitano nilijenga shule mbili za sekondari na kujenga madarasa katika shule kadhaa za msingi na sekondari, na endapo wananchi mtanichagua tena nitaongeza kasi ya kujenga shule hususani katika maeneo ambayo wanafunzi wanalazimika kutembea muda mrefu kufuata elimu," alisema.

Aidha, alisema endapo akichaguliwa hatasubiri fedha za serikali kuu pekee bali atatafuta wadau ili kusaidia kuharakisha maendeleo kwa wananchi ikiwamo upatikanaji wa maji ya uhakika na yanayotosheleza jiji hilo.

Alibainisha mbali na ushirikiano wake na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DUWASA) katika kutekeleza mradi mkubwa wa kutoa maji Mzakwe na visima vya Zuzu, yeye atahakikisha upatikanaji huduma ya maji unaimarika zaidi.

"Kipindi changu cha kwanza cha ubunge kinaisha nimefanya kazi ya kuchimba visima 11 ambavyo vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji," alisema.

Mavunde alisema ataboresha huduma za afya ili wananchi wa Dodoma mjini wapate huduma bora ambapo atahakikisha linapatikana eneo kubwa ambalo litakalotumika kujenga hospitali ya wilaya.

"Pia nitaendelea na mkakati wangu wa kuwainua kiuchumi vijana, wanawake, wazee na watu wenye ulamavu kwa kuwawekea mazingira mazuri ya kufanya biashara na upatikanaji mikopo ili kubadilisha maisha yao," aliahidi.

Kadhalika, kuhusu umeme, aliwaomba wananchi kumpa kura zote ili kukamilisha usambazaji wa umeme kwa kuhakikisha maeneo 34 ambayo hayajafikiwa yanafikiwa na umeme.

"Nitahakikisha barabara zote katika kata 41 zinapitika wakati wote sambamba na kujenga kwa lami barabara za kuanzia Kilimani mpaka Ntyuka, na ile ya kwenda Hombolo kuja mjini," alisema.

Aliwahakikishia wananchi waliopitiwa na miradi mikubwa ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa kimataifa Msalato na ujenzi wa barabara za mzunguko (ring road) kuwa serikali ipo katika mchakato mwisho wa kuwalipa fidia baada ya kukamilika kwa uhakiki.

Pia aliwaomba wananchi kumpigia kura Rais John Magufuli, yeye na madiwani wote wa CCM ili kufanya kazi ya kuwatumikia wananchi.

Naye mgombea ubunge Jimbo la Kibakwe, George Simbachawene, aliwaeleza wananchi wa Msalato kuwa mgogoro kati ya wananchi na Jeshi la Magereza umeisha kwa wananchi kuhamishiwa eneo la Chihikwi.

Awali, aliyekuwa Mbunge wa Shinyanga Mjini, Steven Masele alisema tangu wamejuana na Mavunde miaka 15 iliyopita na kuwa katika kipindi chote alikuwa na kiu ya kuwatumikia wananchi.

## Jamii yatakiwa kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JAMII imetakiwa kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalumu badala ya kuiachia serikali, mashirika na taasisi mbalimbali peke yake.

Mwenyekiti wa umoja wa vijana wa soko la Sabasaba jijini Dodoma, Emmanuel Mtega, aliyabainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wakati akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa kituo cha kulelea watoto cha Cheshire Home Miyuji.

Mtega alisema jamii inalojukumu la kuwasaidia watoto hao, ambao wanaishi katika mazingira magumu ili wajisikie kuwa ni sehemu ya jamii.

Alisema kuwa, watoto wengi wapo katika vituo vingi katika maeneo mbalimbali ya nchi, ambao wanahitaji msaada wa vitu mbalimbali ili kuendesha maisha yao. "Jamii inatakiwa kuwasaidia sana hawa watoto wanamahitaji mengi sana kwani kwa kuwatembelea na kuwapatia msaada itawasaidia kujisikia nao ni sehemu ya jamii na kuwawezesha kutimiza ndoto zao," alisema Mtega.

Pia, alitoa wito kwa serikali kuendelea kuviwezesha vituo vya kulelea watoto, ambavyo hivi sasa vimekuwa vikikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo chakula.

Mmoja wa vijana hao, Wema Sihaba, alisema kuwa vijana wanatakiwa kujitolewa kuwasaidia watoto hao kwa hali na mali na siyo kuendelea kuitegemea serikali pekee yake.

"Mtu yeyote anaweza kuja hapa na kutoa msaada wa kitu chochote ambacho kitawasaidia hawa watoto ambao kwa kiasi kikubwa wanahitaji msaada wetu sisi," alisema Sihaba. Naye katibu wa umoja huo, Dickson Msungu, alisema msaada huo umetokana na wao kuguswa kuwasaidia watoto hao wenye mahitaji maalum ambao wanatunzwa katika kituo hicho bila wazazi wao na jamaa wa karibu.

Vile vile, katibu huyo alisema kuwa msaada huo walioutoa utakuwa endelevu na kuwataka wadau wengine kujitokeza kuwasaidaia watoto hao.

Akitoa shukrani kwa niaba ya kituo hicho Sista Scholastica James, alisema wanashukuru kwa msaada huo kwani umekuja wakati mwafaka.

"Kwa niaba ya kituo nitoe shukrani zetu za dhati na kuwaomba isiwe mwisho na watu wengine wajitokeze kuiga mfano huu, ili kutusaidia watoto kwani tunamahitaji mengi sana kama chakula, sabuni na mavazi," alisema James.



## Sugu aanza kutetea Jimbo Mbeya Mjini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa tiketi ya CHADEMA, Joseph Mbilinyi 'Sugu', ametangaza rasmi kuanza kampeni za kutetea jimbo hilo, hatua inayoibua ushindani kati yake na mgombea wa CCM, Dk. Tulia Akson, ambaye amekwishaanza kampeni za kumng'oa Sugu.

Sugu alitangaza kuanza rasmi kwa kampeni zake juzi alipopanda jukwaani kusalimia wananchi wakati wa mkutano wa kampeni wa mgombea urais kwa tiketi ya CHADEMA, Tundu Lissu, kwenye viwanja vya Ruandanzovwe jijini Mbeya.

Sugu alisema kuwa hakutaka kuanza kampeni zake mapema kwa vile alikuwa akisubiri ujio wa Lissu, hivyo sasa ameamua kuanza kampeni zake ambazo zitamfikisha katika maeneo yote ya Jiji la Mbeya kuomba kura kwa wananchi.

"Sikutaka kuanza kampeni zangu mapema kwa vile nilikuwa namsubiri president (Rais) aje, kwa vile amekuja leo natangaza kuwa sasa nimezindua rasmi kampeni zangu na kuanzia kesho (jana) nitaanza kutembea kwenye kata zote ikiwamo Uyole, Iziwa, Itagano na maeneo yote, hivyo jiandaeni kwa mtiti mkubwa," alisema Sugu.

Alisema kabla ya kuzindua kampeni, alikuwa jijini Dodoma kwenye Ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa zaidi ya wiki moja pamoja na maofisa wengine wa chama hicho kuhangaikia wagombea wa nafasi za udiwani walioenguliwa kwenye mchakato.

Alisema katika jimbo hilo hilo wagombea udiwani wa kata 16 wameenguliwa na wasimamizi wa uchaguzi ngazi ya kata, hivyo kuwafanya wagombea wa CCM kupita bila kupingwa.

Kwa upande wake Dk. Tulia anatarajia kuzindua rasmi kampeni Septemba 9, mwaka huu wakati wa ziara ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye anatarajiwa kufika mkoani Mbeya kwa ajili ya ziara ya kuwanadi wagombea wa CCM.

Pamoja na kwamba Dk. Tulia bado hajazindua kampeni rasmi, lakini ameanza kutembelea baadhi ya kata na kufanya mikutano ya hadhara na wananchi kwa ajili ya kujitangaza.

Mpaka sasa ameshatembelea kata za Iyela na Mwakibete, ambazo ni miongoni mwa kata kubwa zaidi kuliko zingine za Jiji hilo.

# Upatikanaji majisafi wapaa kwa 95%

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UPATIKANAJI wa maji ya bomba katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, umepanda kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 95 baada ya utekelezaji wa mradi wa maji ulioahidiwa na Rais John Magufuli kukamilika.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya, (Mbeya UWSSA), Mhandisi Ndele Mengo, alisema kuwa mradi huo ambao umeanzia kwenye chanzo cha maji cha Shongo mpaka sasa umekamilika kwa asilimia 97.

Alisema katika utekelezaji wa mradi huo, kazi ya ujenzi wa bomba kutoka kwenye chanzo cha maji cha Shongo hadi kwenye tangi katika eneo la Izumbwe na ujenzi wa tangi kubwa lenye ukubwa wa lita za ujazo 1,500 imekamilika kwa asilimia 100.

Mengo alisema pia kaz ya kulaza mabomba kutoka kwenye tangi hadi kwenye makazi ya wananchi katika Mji wa Mbalizi na ujenzi wa vituo vya wananchi kuchota maji katika maeneo mbalimbali ya mji huo na vitongoji vyake pia imekamilika kwa asilimia 100.

"Mpaka sasa tumekamilisha kazi kwa asilimia 97 na tayari maji yameshaanza kuwafikia wananchi hali ambayo sasa imeongeza upatikanaji wa maji katika mji huu wa Mbalizi kutoka asilimia 30 kabla ya kuwapo kwa mradi huu na kufikia asilimia 95," alisema Ndele.

Ndele alisema hali hiyo pia imepuza bei ya maji kwa wananchi kutoka shilingi 500 hadi kufikia shilingi 50 kwa dumu moja la lita 20.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alitembelea mradi huo na kuridhishwa na utekelezaji wake kisha akawataka wananchi kutunza miundombinu hiyo ili iweze kudumu kwa muda mrefu.

"Mradi huu umejengwa kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 3.45, fedha hizi ni ahadi ya Rais Magufuli wakati alipopita hapa Mbalizi Aprili mwaka jana... sasa wito wenu kwenu ni kuitunza miundombinu hii ili idumu na kutusaidia kwa muda mrefu zaidi," alisema Chalamila.

Baadhi ya wananchi wa Mji Mdogo wa Mbalizi walimshukuru Rais Magufuli kwa kutekeleza ahadi yake na kuwaondolea kero ya muda mrefu ya uhaba wa maji katika Mji Mdogo wa Mbalizi.

Maria Seme ambaye ni mamalishe katika Kituo cha Mabasi Mbalizi, alisema kuwa upatikanaji wa maji hayo umesaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara yake na kuokoa muda mwingi uliokuwa ukipotea kwenda kufuata maji mbali.

"Zamani tulikuwa tunanunua maji dumu moja shilingi 500 na maji hayo tulikuwa tunayafuata mbali, lakini sasa napata maji hapa hapa na kwa gharama nafuu ya shilingi 50 tu kwa dumu moja, kwa kweli mradi huu umetusaidia na tunamshukuru sana Rais kwa utekelezaji wa ahadi yake," alisema Seme.

Mradi huo wa maji katika Mji Mdogo wa Mbalizi umetekelezwa kutokana na agizo la Rais Magufuli alilolitoa akiwa ziarani mkoani Mbeya baada ya kusimama katika Mji wa Mbalizi kusikiliza kero za wananchi, ambapo alielezwa kuwa kero kubwa ya mji huo ni uhaba wa maji.



Mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tundu Lissu, akihutubia maelfu ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya juzi, wakati wa uzinduzi wa kampeni za urais Kanda ya Nyansa, kwenye uwanja wa Ruanda Nzovwe. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# EWURA yataka kasi ukusanyaji mapato ya maji

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imezishauri mamlaka za maji za mikoa, wilaya na miji kuongeza kasi ya usambazaji wa dira za malipo ya maji kabla ya huduma kwa wateja.

Lengo ni kuongeza ufanisi wa makusanyo ya fedha na huduma bora kwa wateja.

Ushauri huo ulitolewa na Meneja wa EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Karim Ally, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusiana na umuhimu wa kutumia dira za malipo kabla ya huduma kwa mamlaka za maji zilizopo katika mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Songwe, Njombe, Rukwa na Katavi.

Alisema kuimarishwa kwa huduma hiyo ya malipo kabla ya huduma itakuwa na manufaa makubwa kwa mamlaka za maji na watumiaji wa huduma za maji kutokana na baadhi ya vikwazo ikiwamo baadhi ya wateja kuwa na mzigo wa madeni ya ankra za matumizi ya maji na baadhi ya mamlaka hizo zikituhumiwa kuwabambikizia wateja gharama za ankra ya maji.

"Unajua huduma hii ya malipo kabla ya huduma itaongeza ubora wa huduma kwa wateja wa maji na ufanisi wa kazi wa mamlaka za maji katika kukusanya fedha zinazotokana na matumizi ya maji hususani katika taasisi mbalimbali zikiwamo za serikali na zisizo za serikali," alisema.

Alisema huduma ya malipo kabla ya huduma ina manufaa makubwa sana kwa mteja wa maji kwa kuwa mteja anakuwa na uwezo wa kulipia huduma hiyo ya maji kulingana na mahitaji ya maji au kiwango cha fedha anachokuwanacho kwa wakati huo.

Mhandisi Karim Ally alifafanua mpaka sasa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira ikiwamo ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (MBEYAWSSA), imefanikiwa kufunga dira za malipo ya maji kabla ya huduma zinazofikia 650, Songea imefanikiwa kufunga dira 300, Sumbawanga dira za maji 5, Makambako dira 24, Makete dira za maji 12 na Njombe dira 5.

Alisema mpaka sasa EWURA imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kusimamia utoaji wa huduma bora kwa wateja wa maji katika mamlaka za maji za Njombe, Songea, Sumbawanga, Mbeya na Vwawa - Mlowo ambazo zipo katika makao makuu ya mkoa.

Alisema mbali na kuwapo kwa mamlaka za maji katika ngazi za mikoa, pia EWURA imekuwa ikizisimamia mamlaka za maji za miji midogo ukiwamo mji wa Tunduma na Wanging'ombe.

Alizitaja mamlaka za maji zingine ambazo EWURA inazisimamia katika ngazi za wilaya ni Chunya, Tukuyu, Rujewa na Kasumulu kwa mkoa wa Mbeya na katika Mkoa wa Songwe kuna mamlaka ya Itumba - Isongole na mamlaka ya maji ya Namanyele kwa mkoa wa Rukwa.

Mamlaka zingine za wilaya ni Makete na Ludewa kwa mkoa wa Njombe na mamlaka za maji za Mbinga, Tunduru na Namtumbo kwa mkoa wa Ruvuma.

Ofisa Uhusiano wa Mbeya AWSSA, Neema Stanton, alisema mamlaka hiyo imefanikiwa kufunga dira za maji kwa wateja zikiwamo taasisi za serikali na zisizo za kiserikali, hoteli, vituo vya kuoshea magari na kwa wananchi wa kawaida.

Alisema tangu kufungwa kwa dira hizo kumekuwa na ufanisi mkubwa wa makusanyo ya fedha, ingawa mpaka sasa bado kumekuwa na uhitaji mkubwa wa dira za maji zinazofahamika kama "lipia maji kadri utumiavyo" (LIMAKU) kutoka kwa wateja mbalimbali kwa ajili ya kuzifunga majumbani.

Alisema huduma ya malipo kabla ya maji imekuwa ni msaada mkubwa kwa wateja wengi kwa kuwa wengi wao wamekuwa wakinunua maji kulingana na uwezo wa fedha walizonazo.



# Mwinyi kuwapa wanawake kipaumbele serikalini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Hassan Mwinyi, ameahidi kuwa nafasi nyingi za uteuzi katika serikali atakayoiunda endapo atapata ridhaa za wananchi, atahakikisha wanawake anawapa kipaumbele.

Aliyasema hayo wakati akizungumza katika kongamano maalum la wanawake lililofanyika katika ukumbi wa Amani CCM Mkoa, ambapo mgeni maalum katika kongamano hilo alikuwa Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mwanamwema Shein.

Dk. Mwinyi alisema kuwa ana uhakika mkubwa kwamba CCM itashinda kutokana na wagombea wake kuungwa mkono na makundi yote ndani ya chama hicho wakiwamo wanawake ambao ndio jeshi kubwa la CCM.

Alisema wanawake wamekuwa wakifanya vizuri pale wanapopewa nafasi ya uongozi na wamekuwa wakionyesha uadilifu. Alieleza kuwa katika kampeni zote za CCM, wahamasishaji wakubwa ni wanawake ambao wamekuwa wamoja katika kukiunga mkono na kukitetea chama chao.

Naye Mama Mwanamwema Shein aliwasihi wanawake na wananchi wote kuzingatia umuhimu wa kutunza amani iliyopo na baada ya uchaguzi.

Mama Shein alitoa pongezi zake kwa wanawake kwa kuchagua kaulimbiu ya kongamano hilo isemayo ni "Umoja Wetu Ndio Nguvu Yetu", na kueleza kuwa anakubaliana na kaulimbiu hiyo kutokana na ukweli na umuhimu wake. Alisema wanawake wakiwa pamoja watakuwa na nguvu zaidi ya kufanya uamuzi unaofaa kwa faida yao, na kusisitiza kuwa uamuzi unaofaa hivi sasa ni kuipigania CCM ili ishinde katika nafasi zote za uongozi katika uchaguzi mkuu ujao.

Alisema kuwa mgombea wa urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Dk. Hussein Mwinyi ni mtu makini, mwenye uzoefu mkubwa katika uongozi na anayependa maendeleo.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa CCM (UWT), Gaudentia Kabaka, aliwataka wagombea wote wanawake waliogombea nafasi mbalimbali kuwa kitu kimoja na kufahamu kuwa walioupata ni uteuzi si ushindi na wapo walioshinda kwa kura nyingi, lakini hawakuteuliwa na badala yake wameteuliwa wenye kura kidogo.

Katika kongamano hilo mada mbalimbali zilitolewa ikiwamo "Wanawake Kutokata Tamaa", aliyotolewa Balozi Amina Salum Ali, Waziri wa Biashara na Viwanda, mada ya "Amani na Utulivu" iliyotolewa na Sharifa Abeid Salum kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na mada ya tatu ilihusu "Uzalendo na Mshikamano" iliyotolewa na Catherine Peter Nao, Katibu wa Idara ya Uenezi Zanzibar.



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCM, Dk. Hussein Mwinyi, akisalimiana na mgombea Uwakilishi Jimbo la Dimani, Mwanaasha Khamis Juma, baada ya kumaliza kikao cha wagombea wote wa chama hicho, kilichofanyika Amani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wenye ulemavu wazitaka ZEC, NEC kuwapa haki

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

IDARA ya watu wenye ulemavu Zanzibar, imesema itashirikiana na Tume ya Uchaguzi wa Zanzibar (ZEC) na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata haki ya kupiga kura kwa usalama kama ilivyo kwa watu wasio na ulemavu.

Mkurugenzi wa idara hiyo, Abeda Rashid Abdallah, alisema kupiga kura ni haki ya kila mwananchi aliyekizi vigezo vya tume, hivyo watu wenye ulemavu nao wanahaki hiyo.

Alisema idara hiyo imekua ikishiriki mikutano na tume za uchaguzi na kutoa maoni yao kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata haki ya kuchagua na kupewa kipaumbele kwenye suala hilo.

Alisema kuwa serikali inatambua umuhimu na kuwaamini watu wenye ulemavu kwa kuwa ni sehemu katika jamii, hivyo imetoa mwongozo kila taasisi kuandaa miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Abeda alieleza kuwa katika kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu, idara itahakikisha inaweka mwongozo madhubuti wa maeneo yatakayotumika kipindi cha uchaguzi ili mazingira ya kupiga kura yawe rafiki kwa watu wenye ulemavu.

"Katika kuhakikisha usalama wa watu wenye ulemavu, tunahitaji kupewa vitambulisho maalum vitakavyotumika kama utambulisho wetu ili kupata huduma kwa haraka tunapofika vituoni," alisema.

Akizungumzia ushirikishwaji katika kampeni, alisema wamepeleka ombi lao kwa vyama vya siasa kutaka wapewe eneo maalum ambalo litakuwa salama ili waweze kusikiliza sera zinazotolewa na wanasiasa.

Aidh, aliwataka wazazi, walezi wanaoishi na watu wenye ulemavu kuhakikisha wanakuwa karibu nao katika kipindi cha kampeni ili wasitumike katika kuchochea vurugu na badala yake wawe sehemu ya kuhubiri amani.

Naye Mkuu wa divisheni ya habari na mawasiliano ya umma wa ZEC, Jaala Maakame Haji, alisema katika kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata haki yao ya kupiga kura, wameandaa mafunzo yaliowashirikisha watu wenye mahitaji maalumu ikiwamo walemavu.

Alisema tume hiyo imeanzisha sera ya jinsia na ushirikishwaji wa makundi ya kijamii ya mwaka 2014/ 2015, ambayo inawaongoza namna ya kuwashirikisha kwa usalama ikiwamo watu maalumu.

"Tukiandaa siku ya walemavu wasioona tunashirikisha wakalimani, walemavu wa uoni tunatumia kifaa chenye maandishi ya nukta nundu, pia hutumia karatasi za wagombea kura kama mifano ya kuwaelekeza," alieleza.

Aliwataka watu wenye ulemavu kujitokeza kupiga kura, na kwamba wamejitahidi kutafuta majengo ambayo ni rafiki kwa watu wenye ulemavu kwa ajili ya kutimiza haki zao za msingi ya kikatiba ya kuchagua viongozi wanaowataka.

## Waziri akunwa programu kukabili uhaba wa ajira

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe, amesema Idara ya Elimu ya Watu Wazima imepiga hatua katika kuanzisha programu zinazokwenda sambamba na mahitaji ya jamii kupambana na tatizo la ajira nchini.

Akizungumza kwa niaba yake wakati wa kilele cha maadhimisho ya elimu ya watu wazima huko Chakechake Pemba, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Idrissa Muslim Hija, alisema programu hizo zinaleta matumaini makubwa katika maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Alisema elimu ya watu wazima imeanzishwa na waasisi wa nchi akiwamo Rais wa kwanza wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume na Mwalimu Julius Nyerere ambao waliipa kipaumbele elimu hiyo baada ya kupata uhuru kutokana na kuelewa umuhimu wa elimu ya watu wazima katika maendeleo.

Akizungumzia suala la utekelezaji wa majukumu ya idara hiyo, Waziri Riziki alisema hali hiyo inakwenda sambamba na sera ya elimu ya mwaka 2006 ambayo inaeleza jukumu la uanzishwaji wa programu za elimu ya watu wazima zitakazowanufaisha walengwa kupata waliokosa wakati wa mfumo rasmi wa elimu.

Hata hivyo, aliipongeza idara hiyo kwa hatua kubwa iliyofikia, ambapo hali ya kisomo inaonekana kuimarika katika nchi na kutekeleza kwa vitendo ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Elimu mbadala na watu wazima, Mashavu Ahmada Fakih, alisema lengo la kufanyika maadhimisho hayo ni kufanya tathmini ya hali ya kisomo katika nchi ambapo kwa Zanzibar, na kuwa asilimia 84.2 ya wanaojua wanajua kusoma na kuandika.

Alisema pamoja na kuwapo mafanikio hayo, lakini bado kuna umuhimu kwa mamlaka ya elimu kuendelea kutoa ushirikiano katika kubuni mbinu mbalimbali za kuwasaidia wanakisomo kupata elimu bora pamoja na kuwapo programu mbalimbali za runinga na redio.

Aidha, aliwashukuru viongozi wa mikoa kwa kuwapa ushirikiano wa kutosha kuhakikisha wanafanikiwa katika suala zima la tathmini ya watu wasiojua kusoma na kuandika ili waweze kuwasaidia.

Naibu Mkurugenzi wa Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Tanzania Bara, Mary Watugulu, aliwashauri vijana kujiunga na vituo mbalimbali ili waweze kupata mikopo kwa urahisi itakayosaidia kujikwamua kutokana na suala zima la upatikanaji wa mitaji katika kazi zao.

# Majaliwa afichua siri uwapo amani nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema siri ya Taifa la Tanzania kuendelea kuwa na amani na kimbilio la watu wanaotoka katika nchi ambazo zimepoteza amani ni kwa sababu ya uwapo wa dini, hivyo amewapongeza viongozi wa dini zote nchini kwa kuendelea kuliombea Taifa.

Amesema kuwa kuanzia Serikali ya Awamu ya Kwanza hadi Serikali ya Awamu ya Tano, inaamini kwamba dini ni mkombozi na msingi mkubwa wa amani, mshikamano na utulivu uliopo nchini.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana, katika kongamano maalumu lililoandalia na kituo cha Redio Safina kwa ajili ya kuliombea Taifa na viongozi wake kuelekea kwenye uchaguzi mkuu jijini Arusha.

"Serikali itaendelea kushirikiana na dini zote na Rais Dk. Magufuli anaamini kwamba dini ina mchango mkubwa katika kulifanya Taifa kuendelea kuwa ana amani. Nawashukuru viongozi wa dini nchini kwa kuliombea Taifa na kulifanya liepukane na vikwazo vingi ambavyo vingeleta athari."

Waziri Mkuu alisema nchi iliokolewa kutoka katika majanga mbalimbali ukiwamo ugonjwa wa corona ambao umeendelea kuyasumbua mataifa makubwa yenye uwezo na nguvu duniani kutokana na maombi yaliyofanywa na dini zote baada ya Rais Magufuli kuwaomba Watanzania wafunge siku tatu kumuomba Mwenyezi Mungu aliepushe Taifa na ugonjwa huo.

Aliwasihi viongozi wa dini na wananchi kwa ujumla waendelee kushirikiana katika kuliombea Taifa na wamwombe Mungu aiepushe Tanzania na majanga ili nchi iendelee kuwa na amani.

Akizungumzia kuhusu uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, 2020, Majaliwa alisema siku ikifika wajitokeze kwa wingi na wakachague viongozi bora watakaoweza kuwaletea maendeleo katika maeneo yao.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Iddi Kimanta, aliwahakikishia wananchi wa mkoa huo kwamba mkoa upo salama, na kwamba wajitokeze kwa wingi kushiriki katika kampeni na wasikubali kutishwa na mtu yeyote.



Wakazi wa Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam wakiangalia kazi ya upanuzi wa barabara ya Morogoro kwa ajili ya kupunguza msongamano wa magari ikiendelea juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wanahabari wanafunzi wafundwa

**Na Swalehe Makoye,** SJMC

WANAHABARI wanafunzi wametakiwa kuacha kutengeneza mazingira ya kupewa upendeleo badala yake wajitume kufanya kazi kwa bidii, ili kuwaepusha kujiingiza kwenye mtego wa rushwa ya ngono.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA-TAN), Salome Kitomari, wakati akitoa mada katika mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kutambua nafasi zao wanafunzi wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC).

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Jukwaa la Wahariri duniani (WAN-IFRA) chini ya mradi wa Wanawake na Habari (Women In News), inaolenga kuwaandaa wanawake kushika nafasi za maamuzi ndani ya vyombo vya habari

Alisema yamekuwapo malalamiko ya wanafunzi au waandishi wachanga kusumbuliwa, lakini zipo tabia za wanafunzi husika kutengeneza mazingira ya kutega wahusika, jambo ambalo ni baya sana.

"Tujifunze kujijengea uwezo wa kazi, tutumie vyema uwezo na elimu tuliyonayo, usikubali kupendelewa bali simama kwa miguu yako mwenyewe kuhakikisha unafanyakazi kwa kiwango cha juu ambacho kitakutambulisha kokote uendako ukisubiri kupendelewa lazima utumie njia ya mkato," alisema.

"Mafunzo haya yanalenga kuongeza wanawake katika vyumba vya habari hasa kwenye nafasi za uongozi na maamuzi kwa kuwaandaa wanawake tangu wakiwa vyuoni kwa kuwapa ujasiri na uzoefu kwani wanawake wanaweza," alisema Kitomari.

Katika mafunzo hayo, pia wanafunzi hao walifundishwa utngenezaji wa video ndogondogo za podcast, namna ya kujitangaza na kujitambulisha kwenye jamii kwa namna ya kujitofautisha.

Mengine ni uandishi wenye kuleta suluhisho katika jamii, kumjua na kukabiliana na bosi wa aina yeyote.

Awali, Mkurugenzi wa Jukwaa la Wanawake Wanahabari (WRIFO), Chelu Matuzya, aliwataka wanafunzi hao kuanza kutumia vyema fursa wanazopata hasa wanapofanya mazoezi kwa vitendo ndani ya vyombo vya habari, aonyeshe ubunifu na uchapakazi kwa kuwa ndiyo silaha yao.

Aidha, aliwataka wanafunzi hao kuwa makini na kila wanachorusha kwenye mitandao ya kijamii, na badala yake watumie kufanya mambo ambayo yatawaongezea thamani kitaaluma na kulinda utu wao.

# Wananchi wampa jukumu mgombea iwapo atachaguliwa

**Na Shaban Njia,** MBOGWE

WAKAZI wa Halmashauri ya Mbogwe, mkoani Geita, wamemtaka mgombea wa jimbo hilo kupitia CCM, Nicodemas Maganga, iwapo atapata ridhaa ya kuchaguliwa kuongoza jimbo hilo asimamie ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Lulembela ili kudhibiti vifo vya wajawazito na watoto.

Walisema, kata hiyo ina zaidi ya wakazi 40,000 na zahanati moja ambayo haitoshelezi mahitaji kwa wananchi na kusababisha kuwapo kwa msongamano mkubwa wa wagonjwa wanaofika kituoni hapo kupata matibabu, huku wengi wakiwa wajawazito na watoto.

Maombi hayo waliyatoa jana wakati wa ufunguzi wa kampeni za kiwilaya yaliyofanyika katika kijiji na kata ya Lulembela, Halmashauri ya Mbogwe na kuhudhuriwa na viongozi wa CCM, Mkoa wa Geita pamoja na mgombea wa Jimbo la Chato, Dk. Medard Kalemani.

Mudahi Balele, mkazi wa jimbo hilo alisema kuwa, vifo vya wajawazito na watoto ni tatizo la kudumu katika Halmashauri ya Mbogwe hasa pembezoni mwa mji na kuongeza kwa mujibu wa takwimu za mwaka jana 2019/20, vifo vya wajawazito kwa kukosa matibabu kwa wakati vilikuwa 84.

Mkazi mwingine, Simon Kasanga alidai, vifo hivyo vinatokana na msongamano wa wagonjwa katika zahanati iliyopo ya Lulembela, ili kutokomeza vifo hivyo anatakiwa kusimamia ujenzi wa kituo cha afya katika kata hiyo itakayosadia kupunguza msongamano wa wagonjwa na kusafiri umbali mrefu kwenda Hospitali ya Wilaya kwa matibabu zaidi.

Naye Martha Luzari, mkazi wa Lugunga alisema, wajawazito wanashindwa kuhudhuria kliniki na kujua maendeleo ya mtoto tumboni kama ni mzima ama la kwa madai ya lugha za matusi zinazotolewa na baadhi ya wauguzi hasa mjamzito anapochelewa kuanza kliniki.

"Sio kwamba hatutaki kuhudhuria kliniki, tunashindwa kuhudhuria kwa kuogopa kurushiwa matusi na wauguzi hasa pale tunapochelewa kuanza kliniki yetu. Hii imesababisha wengi wetu kuwa waoga na kuchukua maamuzi ya kujifungulia majumbani na kuwa na uzazi ambao sio salama," alidai.

Aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Agustino Masele, alimtaka mgombea Maganga kusimamia na kutekeleza miradi aliyoibua na kushindwa kukamilika kwa wakati hasa katika sekta ya elimu, afya na maji ili kutoa huduma kwa wananchi.

Akijibu maombi hayo, Maganga alisema, endapo atapata ridhaa na kuwaongoza wananchi, atahakikisha anasimamia ujenzi wa kituo cha afya na hayo yote yatawezekana endapo watampatia kura za ndio mgombea urais, mbunge na diwani.

Kuhusu lugha za matusi kwa wagonjwa, aliahidi kukaa vikao na Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mbogwe na wasimamizi wa vituo vya afya na zahanati kutatua tatizo hilo ili wajawazito waendelee kuhudhuria kliniki bila woga.

HABARI KITAIFA

# Watumishi washauriwa kuchunguzwa afya zao

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WATUMISHI wa taasisi za serikali wametakiwa kuwa na utaratibu wa kuchunguza afya zao mara kwa mara, ili kugundua matatizo yao, jambo ambalo litasaidia kupata matibabu mapema.

Hayo yameelezwa na Ofsa Mdhamini wa Wizara ya Afya, Pemba Shadya Shaban Seif, wakati akizindua uchunguzi wa afya kwa wafanyakazi wa taasisi mbalimbali katika Ofisi za Serikali Gombani Chakechake Pemba.

Alisema imeonekana kwamba wafanyakazi wengi hawana muda wa kufika hospitali kuchunguza afya zao kutokana na muda mwingi kuwapo kazini na ndio maana wizara kwa kushirikiana na madaktari kutoka China wakaamua kuandaa mpango wa kuwafuata kuwapima afya.

"Wafanyakazi hawana muda wa kwenda hospitali kupima afya zao, muda wote wapo kazini, hivyo tumeamua kuwasogezea huduma hizo karibu, ili wajue afya zao," alisema mdhamini huyo.

Aidha, aliwahimiza wafanyakazi hao kufanya mazoezi mara kwa mara na kupunguza kula vyakula vya mafuta, ili kuepuka ugonjwa wa shindikizo la damu ambao unawapata watu wengi.

"Kuleni zaidi vyakula vya matunda kwa kuimarisha afya zanu, epukeni kula vyakula vya mafuta, kwani hivyo sio vizuri kwa afya," alisema Seif.

Naye kiongozi wa timu ya madaktari kutoka China wanaofanya kazi katika Hospitali ya Abdalla Mzee mkoani Pemba, Dk. Yuan Tongzhou, alisema lengo la kuwafuata wafanyakazi hao kwa kuwafanyia uchunguzi na matibabu ni baada ya kuona kwamba wamekuwa na majukumu ya kuwatumikia wananchi, hali ambayo inawasababishia kukosa muda wa kwenda kupima afya zao.

"Tangu tulipofika katika hospitali hii tumekuwa na utaratibu wa kuwafuata wananchi vijijini kuwachunguza afya zao, lakini leo hii tumewafuata na hawa wafanyakazi kwani na wao hawana muda wa kuifuata huduma hii, jambo ambalo ni hatari kwao," alisema daktari huyo.

Ofisa Mdhamini Wizara ya Katiba na Sheria Pemba, Mattar Zahor, alipongeza uongozi wa Wizara ya Afya kuwafanyia uchunguzi wafanyakazi wake na wananchi kwa ujumla, na kumhakikishia kutoa ushirikiano kwenye shughuli za kiutendaji za utumishi wa umma.

Naye Ofisa Uendeshaji Tiba kutoka Wizara ya Afya Pemba, D. Yussuf Hamad Iddi, alisema utoaji huo wa matibabu ni mwendelezo wa madaktari awamu ya sita kuwafikia wananchi kisiwani Pemba.

# JPM apewa 5 mazingira wezeshi kwa wawekezaji

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS John Magufuli amepongezwa kwa kujenga mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji nchini.

Pongezi hizo zilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Total Tanzania, Jean Schoepp, wakati wa uzinduzi wa kituo kipya cha mafuta cha Total Mchigani, Goba jijini Dar es Salaam kinachomilikiwa na mzawa.

"Tunampongeza Rais Magufuli na serikali yake kwa kujenga mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji ambao umesaidia hata kampuni ya mafuta ya Total kuendelea kuwekeza Tanzania, na pia kuwajengea uwezo Watanzania kupata fursa za kuingia katika biashara ya vituo vya mafuta vya kiwango cha kimataifa," alisema Schoepp.

**Total inalenga kumfikia kila Mtanzania na kuwapatia wananchi fursa ya kufurahia huduma kutoka katika kampuni hiyo.**

Alisema Total inalenga kumfikia kila Mtanzania na kuwapatia wananchi fursa ya kufurahia huduma kutoka katika kampuni hiyo.

Akizungumzia kuhusu Total, Mkurugenzi wa Sheria na Uhusiano wa Total, Marsha Kileo, alisema mbali na kuwekeza katika sekta ya mafuta, pia kampuni hiyo imekuwa ikisaidia kutoa ujuzi kwa Watanzania pamoja na mbinu za namna ya kumiliki vituo vya mafuta.

Kwa upande wake, mmiliki wa kituo cha mafuta cha Total eneo la Goba, Frank Malle, aliishukuru kampuni hiyo kwa kumpatia mbinu ya kuwekeza katika sekta hiyo.

"Naishukuru sana Total kwa kuwekeza katika sekta hii muhimu katika nchi yetu na kutupa na sisi ujuzi wa namna ya kuingia katika biashara hii. Nakumbuka tulikuwa tunataka kuuza hii ardhi, lakini viongozi wa kampuni hii walitushauri tusiiuze, na leo hii na sisi kama Watanzania tumefanikiwa kumiliki kituo cha mafuta," alisema Malle.



Mkurugenzi Mtendaji wa Total Tanzania B, Jean Franchois Schoepp (mwenye suti), akiwa na Mhandisi Frank Malle, mmiliki wa kampuni ya F.S Mshuwa Co, wakifurahi baada ya kukata utepe, kuzindua kituo kipya cha huduma ya mafuta cha kampuni hiyo, Mchigani eneo la Goba jijini Dar es Salaam wiki iliyopita. **MPIGAPICHA WETU**

# TANESCO yatoa elimu umeme vijijini

**Na Mwandishi Wetu,** RUKWA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Rukwa limeamua kufanya uhamasishaji na utoaji elimu kwa wananchi wa vijiji vilivyopatiwa mradi wa usambazaji umeme vijijini (REA), ili wahamasike na kufunga umeme kwenye nyumba zao na kuutumia kwa uzishaji mali.

Uhamasishaji huo ulitolewa jana na mwakilishi kutoka Idara ya Masoko wa shirika hilo, Sylvester Matiku, kwa kushirikiana na Ofisa Uhusiano, Saidy Mremi.

Akizungumza jana wakati wa uhamasishaji huo, Matiku alisema wamefanikiwa kuhamasisha na kutoa elimu ya huduma za umeme kwa vijiji zaidi ya 25 vilivyoko wilaya za Sumbawanga, Laela, Kalambo na Nkasi.

Alitaja baadhi ya elimu walizowapa ni pamoja na kujua taratibu za kuunganisha umeme, elimu ya usalama, ulinzi wa miundombinu, tahadhari ya ajali za umeme, elimu ya matumizi bora ya umeme na jinsi ya kujiepusha na matapeli (vishoka).

Alitaja baadhi ya vijiji vilivyonufaika na elimu hizo ni Kaengesa, Lyapona, Mpombwe, Kapozwa, Kalambo, Kilewani, Kalemashi, Katili na Kipanga.

Vingine vitakavyonufaika ni Kazovu, Korongwe, Kabwe, Mbende, Katani, Zimba, Nankanga, Kizumbi, Mpui, Miangalua, Lowe, Kalambezi, Tunko, Kianda na Lowe.

Kwa upande wake Ofisa Uhusiano Saidy Mremi, alisema mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa kwanza unatekelezwa na mkandarasi wa NAKUROI, ambapo umewezesha vijiji 120 kupata huduma za umeme.

Alisema mradi umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90, na wananchi waliounganishiwa umeme kwa njia moja na njia tatu ni zaidi ya 3,500.




# SANE AONYWA BAYERN

**MUNICH,** Ujerumani

LEROY Sane ameonywa kutarajia "presha tofauti" pale Bayern Munich na Mehmet Scholl.

Winga Sane amerudi Ujerumani kuelekea msimu wa 2020-21, akiwa ameiunga na Bayern kutoka Manchester City kwa dili lililoripotiwa kuwa pauni milioni 54.8.

Licha ya Ujerumani kushinda mataji mawili ya Ligi Kuu ya England pamoja na EFL na FA chini ya Pep Guardiola, Sane alihamia Bayern timu ambayo msimu uliopita ilishinda mataji matatu.

Scholl, ambaye alicheza mechi 469 kwa Bayern kati ya mwaka 1992 na 2007, anahisi Sane mwenye umri wa miaka 24, anahitaji kujua matarajio katika mazingira mapya.

"FC Bayern ni klabu ya aina yake, kuna hali maalumu," alisema akiliambia jarida la Bild. "Hapa ni tofauti, presha tofauti. Unatakiwa kuwa makini kama mchezaji kijana.

"Lakini kama atajipanga vizuri, halitakuwa jambo gumu kwa upande wake."

Sane alianza kucheza kwa mara ya kwanza baada ya miezi 13 Alhamisi wakati alipokuwa kwenye kikosi cha Ujerumani kilichotoka sare ya kufungana 1-1 dhidi ya Hispania katika mchezo wa Ligi ya mataifa ya UEFA.

Kwa mara mwisho alianza kwenye kikosi cha City kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii Agosti mwaka 2019, wakati alipoumia mguu.

# Klopp amtarajia Minamino kutamba EPL

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp ana matumaini, Takumi Minamino anaweza kukibeba kiwango chake anachokionyesha kwenye maandalizi hadi kwenye msimu mpya baada ya kung'ara wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa 7-2 katika mchezo wa kirafiki dhidi ya Blackpool.

Usajili huo wa Januari kutoka Salzburg alifunga kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii wakati wakifungwa na Arsenal na pia alifunga dhidi ya Blackpool pale kwenye dimba la Bloomfield Road, Jumamosi.

Minamino alianza nyuma ya Roberto Firmino katika mfumo wa 4-2-3-1 na alimtengenezea bao la tatu kiungo huyo wa kimataifa wa Brazil wakati wakitoka nyuma kwa mabao 2-0.

Na Klopp anakiona kipaji cha mchezaji huyo wa kimataifa wa Japan anaweza kuwa kwenye kiwango cha kuvutia kwa Liverpool msimu ujao wakati wakianza kutetea taji la Ligi Kuu dhidi ya Leeds United.

"Nina matumaini anaweza kuendelea kujiamini," alisema Klopp akiiambia tovuti ya klabu hiyo. "Na hivyo ndio kitu ambacho nina kitumaini.

"Ni muhimu kwa Taki na muhimu kwa upande wetu, lakini ni suala linalotuhusu wote, hivyo naamini kiwango chake kitazidi kuimarika, hicho ndio ninachokiona."






# Kocha Ujerumani asikitika Havertz kujiunga Chelsea

**MUNICH,** Ujerumani

UHAMISHO wa Kai Havertz kutoka Bayern Leverkusen kwenda Chelsea ni mbaya kwa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, kwa mujibu wa kocha wa timu ya taifa ya Ujerumani, Joachim Low.

Ujerumani ilimruhusu Havertz kuondoka kwenye kambi ya mazoezi mjini Stuttgart Ijumaa kwenda kukamilisha usajili wake kule Chelsea, ambako amesaini mkataba wa miaka mitano.

Blues hao pia wamesajili nyota wengine kutoka Bundesliga, Timo Werner wa RB Leipzig kuungana na nyota wengine kama Hakim Ziyech, Ben Chilwell, Thiago Silva na Malang Sarr.

Low alihuzunishwa kuona Havertz akiondoka Bundesliga, lakini ana matumaini hilo linaweza kumsaidia kuimarika zaidi na kuwa na mchango mkubwa kwa timu ya taifa.

"Naona kama ni jambo hasi wakati vipaji vikubwa kama Kai havipo tena Bundesliga," alisema Low akiwaambia waandishi wa habari Jumamosi.

"Lakini naona kuna faida chanya. Kucheza nje kunawafanya wachezaji kuimarisha vipaji vyao.

"Nafikiri ni muda muafaka kwa Kai, na pia kwa Werner. Kama watajiimarisha zaidi litakuwa jambo zuri zaidi kwa timu ya taifa."

HABARI MICHEZO

# Giggs: Nitaendelea kumchagua Bale

**CARDIFF,** Wales

GARETH Bale ataendelea kuchaguliwa na Ryan Giggs kwenye kikosi cha Wales licha ya kupata nafasi ndogo ya kucheza kule Real Madrid.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ambaye hana nafasi ya kucheza ndani ya kikosi cha Madrid alitolewa nje kipindi cha pili wakati Wales wakiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Finland Alhamisi.

Giggs alibainisha baada ya mchezo huo kwamba kutolewa nje kwa Bale kulipangwa, ambaye amecheza jumla ya dakika 100 tangu Februari kabla ya kuelekea Helsinki.

Hata hivyo, bosi huyo wa Wales amesema hana shaka na mchezaji huyo kwani ana imani naye kubwa.

"Kwa hali ilivyo, haitabadilika. Mara zote nina furaha kuwa na Gareth wakati anapokuja hapa," amesema Giggs.

"Ni mtu muhimu kwa timu yetu hasa katika kambi na kila mmoja anamwangalia yeye. Kama kila mmoja wetu anataka kuwa naye kikosini mwetu.

"Sina tatizo lolote na Gareth na ataendelea kuwa sehemu ya kikosi changu kwa hakika kabisa tutaendelea kuwa naye.





# MBAPPE HATIHATI KUIVAA CROATIA

**STOCKHOLM,** Ufaransa

KOCHA Mkuu wa Ufaransa, Didier Deschamps amesema hatakuwa tayari kujiweka kwenye hatari ya kumtumia Kylian Mbappe wakati mabingwa hao wa Kombe la Dunia wakitarajia kucheza dhidi ya Croatia.

Mbappe alifunga bao la ushindi, lakini aliumia kifundo cha mguu wakati Ufaransa wakiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Sweden kwenye mchezo wa Ligi ya Mataifa ya UEFA wa kundi A3, Jumamosi.

Nyota huyo wa Paris Saint-Germain, ambaye awali aliumia kabla ya kucheza kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, alitolewa nje dakika ya 13 kwenye mchezo huo uliopigwa mjini Stockholm.

Deschamps aliulizwa kuhusu ufiti wa Mbappe wakati wakijiandaa kuivaa Croatia kesho Jumanne.

"Alikuwa vizuri kwenye mchezo," alisema Deschamps akiwaambia waandishi wa habari.

"Aliumia kwenye kifundo cha mguu. Aliendelea kucheza, lakini sitaweza kuchukua hatari ya kumchezesha. "Tutaona namna mambo yatakavyokuwa. Hata kwa wachezaji wengine, sitaki kuhatarisha afya yake.

"Ngoja tusubiri hali yake itakavyokuwa. Sina uhakika kama atacheza Jumanne dhidi ya Croatia."

# Ronaldo hana uhakika kucheza dhidi ya Sweden

**LISBON,** Ureno

CRISTIANO Ronaldo bado hana uhakika wa kuichezea Ureno kwenye mchezo wa kesho Jumanne wa Ligi ya Mataifa ya UEFA dhidi ya Sweden baada ya kuukosa ule wa ushindi wa 4-1 dhidi ya Croatia baada ya kuumia kidole.

Kocha wa kikosi cha Ureno, Santos alibainisha hali ya Ronaldo kuelekea mchezo dhidi ya Croatia utakaopigwa kesho.

Ureno haikuwa na wakati mgumu licha ya kukosekana kwake pale kwenye dimba la Dragao, kwani Joao Cancel, Diogo Jota, Joao Felix na Andre Silva kila mmoja alifunga dhidi ya Croatia kabla ya Bruno Petkovic kufunga la kufutia machozi.

"Nilimpumzisha yeye. Kama angekuwa fiti ningemwanzisha kwenye kikosi cha kwanza ili acheze," alisema Santos akiiambia RTP.

"Leo (jana) alifanya mazoezi vizuri, na alionekana kujisikia vizuri na tutaangalia kama ataweza kucheza kwenye mchezo unaokuja.

"Hana majeruhi makubwa kwa sasa, lakini bado hayuko fiti."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# THIAGO AIKANA RASMI LIVERPOOL

●●● Kwa upande wangu, akili yangu haijawahi kuliwaza jambo hilo na hivyo sina cha kusema...

**MUNICH,** Ujerumani

KIUNGO wa Bayern Munich, Thiago Alcantara anaonekena kujiweka mbali na ripoti kwamba anataka kujiunga na mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Liverpool.

**Thiago aling'ara wakati Bayern ikimaliza msimu kwa ushindi wa 1-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain mwezi uliopita, lakini mara kwa mara amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Liverpool.**

Hata Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bayern, Karl-Heinz Rummenigge, alisema anatarajia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 anaondoka, lakini Thiago amesema amnaiona klabu hiyo kama "nyumbani" baada ya sare ya 1-1 dhidi ya Ujerumani mjini Stuttgart.

Akizungumza na waandishi wa habari akiwa na kocha wa timu ya taifa ya Hispania, Luis Enrique Jumamosi, nyota huyo wa zamani wa Barcelona alionekana kutolijua hilo.

"Kamwe sijawahi kusema kwamba naondoka Bayern," alisema. "Kila mwaka nyinyi (waandishi wa habari) mnaniweka kwenye klabu tofauti.

"Kwa upande wangu, akili yangu haijawahi kuliwaza jambo hilo na hivyo sina cha kusema kuhusu hilo.

"Kamwe sijali sina mpango na habari za uvumi. Ninachoangalia mimi kwa sasa ni hapa nilipo."

Aidha, Thiago alibainisha kuwa majaliwa yake kwa sasa ni kuona Bayer Munich ikirudi vizuri kwenye Ligi Kuu msimu huu mpya wa 2000-21 na hajawahi kuwaza kingine.

"Kwa sasa tuzungumze kuhusu Bayern, hizo timu mnazonipa wala sijawahi kuzifikria wala kutamka lolote.

Thiago ni zao kutoka akademi ya Barceloma La Masia ambako ndiko alikokulia kabla ya kuondoka pale Camp Nou.

## ZISIKUPITE

### HAWANA UHAKIKA NA BALE

REAL Madrid bado haijaondoa uwezekano wa winga wake, Gareth Bale raia wa Wales mwenye umri wa miaka 31 kuondoka klabuni hapo kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Sport)***

### GRIEZMANN AWANIWA EPL

MANCHESTER United, Arsenal na Liverpool zipo kwenye mbio za kuwania kumsajili mshindi wa kombe la Dunia na Ufaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 29 kutoka Barcelona, baada ya maamuzi ya Lionel Messi kubaki pale Nou Camp. ***(Mail)***

### YATAJA BEI YA WIJNALDUM

LIVERPOOL imeiambia Barcelona itawagharimu pauni milioni 15 kama wanataka kumsajili kiungo wao, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 29 raia wa Uholanzi. ***(Mirror)***

### GIGGS AMPA SOMO AMPADU

KOCHA wa timu ya Taifa ya Wales, Ryan Giggs anaamini mlinzi, Ethan Ampadu mwenye umri wa miaka 19 anaweza kufanya maamuzi makubwa kuhusu kukaa kwake pale Chelsea kwa sababu ya kukosa muda mwingi wa kucheza. ***(Sky Sports)***

### NEWCASTLE YATOA OFA

NEWCASTLE imetoa ofa ya pauni milioni 20 kwa straika wa Bournemouth, Callum Wilson na wanataka kukamilisha dili hilo kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu ya England. ***(Sunderland Echo)***

### POGBA ANATAKA KURUDI JUVE

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 27, anataka kurudi Juventus, ndio maana bado hajasaini mkataba mpya pale Old Trafford - huku mkataba wake wa sasa ukiwa unamalizika mwaka 2021. ***(Tuttosport)***

### AIBUA UVUMI WA REGUILON

GOLIKIPA wa Manchester United, David de Gea ameposti picha ya raia mwenzake wa Hispania, Sergio Reguilon kwenye ukurasa wake wa Instagram, na kusababisha uvumi kwamba, mlinzi huyo wa Real Madrid mwenye umri wa miaka 23 anaelekea Old Trafford. ***(Manchester Evening News)***

### YAKARIBIA KUMSAJILI MENDY

MAZUNGUMZO kati ya Chelsea na Rennes juu ya usajili wa golikipa, Edouard Mendy mwenye umri wa miaka 29 raia wa Senegal yamefikia katika hatua nzuri. ***(Sun)***

### SPURS YAJITOSA KWA HUGHES

KLABU ya Tottenham Hotspur inaandaa ofa ya pauni milioni 13 kwa ajili ya kumsajili kiungo wa Watford, Will Hughes mwenye umri wa miaka 25. ***(Mirror)***

### DAJAKU AWANIWA SHEFFIELD

KLABU ya Sheffield United ina nafasi nzuri zaidi ya kumsajili fowadi wa Bayern Munich, Leon Dajaku mwenye umri wa miaka 19, kwa mkopo kutoka Swansea na Torino pia wameonyesha nia ya kuwania kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani. ***(Goal)***

HABARI MICHEZO

# Anna Kibira kuzikwa leo

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama cha Netboli (Chaneta), Anna Kibira anazikwa leo Jumatatu, katika makaburi ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Kibira aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama hicho mwaka 2017, alifariki dunia juzi usiku baada ya kusumbuliwa kwa muda mrefu na maradhi ya presha iliyosababisha kupooza na mwisho kusababisha kifo chake.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Katibu Mkuu wa Chaneta, Judith Ilunda, alisema msiba unafanyika nyumbani kwa mtoto wake maghorofa ya Keko na leo anatarajia kupumzishwa katika nyumba yake ya milele.

Alisema kabla ya kwenda kumpumzisha mpendwa wao katika nyumba yake ya milele, kutakuwa na misa kwenye kanisa la KKKT lililopo maeneo ya Keko jijini Dar es Salaam.

"Chaneta tumepokea kwa masikitiko makubwa kifo cha Kibira, alikuwa na mchango mkubwa katika kukuza mchezo wa netboli, msiba umetugusa sana kwani hata wakati anafariki dunia juzi (majuzi) usiku, nilikuwapo hivyo itoshe kusema Mungu ampumzishe kwa amani.

Kibira alikuwa mwalimu, mlezi sababu alinikuza tangu mdogo nikiwa nacheza, baadaye akawa katibu mkuu wa Chaneta 2013 akawa Mwenyekiti, huku nikiwa mjumbe wa kamati ya utendaji kabla ya 2017 kupumzika na shughuli za michezo," alisema Ilunda.

Alisema baada ya kupata maradhi ya kusumbuliwa na presha kali na iliyosababisha kupooza aliamua kupumzika na shughuli zote za michezo.

# KMKM yasajili 3

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya KMKM inayoshiriki Ligi Kuu ya Zanzibar imesajili wachezaji watatu kwa ajili ya msimu mpya wa 2020-21.

Wachezaji hao ni Mwinyi Haji Ngwali kutokea Singida United, Matteo Anton kutoka Polisi Tanzania na golikipa namba moja wa timu ya Taifa ya Zanzibar, Ahmed Ali Suleiman ambaye ametokea klabu ya Malindi.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa timu hiyo ya KMKM, Ame Msimu, alisema lengo lake ni kusajili wachezaji wazuri na watakayoitumikia timu katika msimu wa 2020/2021 ambao kwake yeye anauona kuwa ni msimu mgumu. Alisema uongozi wa timu hiyo kusajili wachezaji hao watatu kwa hatua ya awali wamefanya jambo zuri kutokana na kila timu hivi sasa inasajili wachezaji wazuri ambao watafanya vizuri katika timu zao hii ni kutokana na msimu huu kuwa na timu 12 ambazo zitashiriki ligi hiyo.

Alisema kwa upande wake kocha huyo anakubaliana na uongozi wa KMKM kwa usajili huo, hivyo amesema timu hiyo inahitaji nafasi nyingine mbili za kusajili ambazo ni kiungo wa kati pamoja na mlinzi.

Hata hivyo, alisema kuwa timu hiyo inatarajia kuanza mazoezi yake mapema Jumatatu hii, ili kujiandaa na msimu wa 2020/2021 ambao bado Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar hajasema lini msimu mpya wa ligi utaanza.

# UNYANYEMBE, MAPINDUZI ZAPANDA DARAJA WANAWAKE

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TIMU za ES Unyanyembe kutoka mkoani Tabora na Mapinduzi Queens ya Njombe zimepanda daraja na kucheza Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu ujao baada ya kufanya vema katika mechi zake za hatua ya nusu fainali ya Ligi Daraja la Kwanza zilizofanyika kwenye Uwanja wa Fountain Gate Academy jijini hapa jana.

**Mapinduzi Queens walikuwa wa kwanza kupata tiketi hiyo baada ya kuwafunga Evergreen Queens ya jijini Dar es Salaam mabao 3-0 katika mechi ya nusu fainali ya kwanza iliyokuwa na ushindani muda wote.**

Mapinduzi Queens ilienda mapumziko ikiwa mbele kwa mabao 2-0, na ikiporejea kipindi cha pili ilipata bao la tatu ambalo liliwahakikishia tiketi ya kupanda daraja.

ES Unyanyembe yenyewe ilifuzu hatua hiyo baada ya kuwafunga Ilala Queens ya Dar es Salaam mabao 3-0, magoli yote yakifungwa katika dakika 45 za kwanza za mchezo huo.

Timu hizo zimechukua nafasi ya Marsh Queens pamoja na Panama Queens ambazo zilishuka daraja baada ya kufanya vibaya katika msimu uliopita wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ambayo inashirikisha klabu 12.

Ofisa Mashindano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Baraka Kizuguto, alisema jumla ya wachezaji 26 wameteuliwa katika kikosi cha "Dream Team" ambacho kitanolewa kupata nyota watakaojiunga na timu za taifa za wanawake.

Kizuguto alisema mashindano yalishirikisha mabingwa wa timu za mikoa 16 na yamefanyika kwa kiwango cha hali ya juu.

Aliongeza anaamini ushindani ulioonyeshwa utazidi katika msimu ujao kwa sababu kila mkoa una kiu ya kupata klabu inayoshiriki kwenye Ligi Kuu ya Wanawake.

Ligi hiyo iliyoandaliwa na TFF ilimalizika jana na mgeni rasmi alikuwa ni Rais wa Shirikisho hilo, Wallace Karia pamoja na Mkurugenzi wa Fountain Gate Academy, Joseph Makau.



Msanii wa muziki wa kizazi kipya, Mwasiti Almas, akitumbuiza kwa wajasiriamali wakati wa kongamano la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa maendeleo endelevu lililofanyika Kigamboni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Azam, Polisi Tanzania zatambiana*

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwamo mechi yao dhidi ya Polisi Tanzania itakayopigwa leo uwanja wa Azam Complex.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Vivier alisema kikosi chao kipo tayari kwa ajili ya mechi hiyo pamoja na zilizokuwa mbele yao kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

Alisema maandalizi wamefanya vizuri na kufanyia kazi mapungufu waliyoyaona katika michezo yao ya kirafiki na sasa wapo fiti kwa ajili ya ligi hiyo.

"Kiujumla ligi itakuwa ni ngumu, tumejiandaa kutafuta pointi muhimu katika kila mechi, tunawaheshimu wapinzani wetu, tumejipanga kutafuta matokeo kwa kila mechi ili kufikia malengo yetu," alisema Vivier.

Naye kocha wa Polisi Tanzania, Hamsini Malale alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya kutafuta alama muhimu katika mechi hiyo.

"Tumejipanga, vijana wangu wana ari ya kufanya vizuri, tunacheza usiku hivyo haitakuwa kigezo kwetu kupoteza pointi, tunawaheshimu Azam wamefanya usajili mzuri lakini hata sisi tumeboresha timu yetu," alisema Malale.


Alisema muda wa usiku ambao mechi itachezwa haitawaathiri na kuzuia kupata matokeo mazuri katika mchezo huo wanaocheza ugenini.

Azam leo inashuka dimbani wakiwa wenyeji katika uwanjani huo, ukiwa ni mwendelezo wa Ligi Kuu Bara iliyoanza jana kwa timu mbalimbali kucheza katika viwanja tofauti.

# Michezo

Jumatatu Septemba 7, 2020

Nipashe

Thiago aikana rasmi Liverpool UKURASA 22



Mzamiru Yassin akishangilia na John Bocco baada ya kufunga bao la pili la Simba wakati wa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu uliopigwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, jana Jumapili. Simba iliibuka na ushindi wa mabao 2-1. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA YAANZA KWA USHINDI WA MBINDE

## ●●● Namungo, Biashara, Dodoma zatakata, Bigirimana wa kwanza kufunga Ligi Kuu...

**Na Isaac Kijoti,** MBEYA

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, wameanza msimu mpya kwa ushindi wa mbinde tofauti na msimu uliopita baada ya kushinda 2-1 kwa tabu dhidi ya wageni wa ligi hiyo, Ihefu FC.

**Msimu uliopita ambao ulianza Agosti 29, mwaka jana, Simba iliuanza kwa ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya JKT Tanzania katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Taifa/Mkapa, wafungaji wakiwa Meddie Kagere aliyetupia mawili na Miraji Athumani moja.**

Katika mechi ya jana iliyopigwa Uwanja wa Sokoine jijini hapa, huku ikichezeshwa na mwamuzi Martin Saanya, safu ya ushambuliaji ya Simba ikiongozwa na nahodha John Bocco, Clautos Chama, Bernard Morrison na Hassan Dilunga, ilianza kwa kasi.

Lakini safu ya ulinzi ya mabingwa watetezi hao ikiwa chini ya mabeki wa kati, Mkenya Joash Onyango na Kennedy Juma wakisaidiwa pembeni kulia na Shomary Kapombe na kushoto akiwa Mohammed Hussein 'Tshabalala' ilicheza kwa kujiamini na licha ya makosa madogo madogo.

Dakika ya 10 tu, Simba ilipata bao la kuongoza kupitia kwa Bocco akiukwamisha mpira wavuni kwa mguu wa kulia akiitendea haki pasi ndefu ya Mzamiru Yassin.

Lakini bao hilo lilidumu kwa dakika nne tu baada ya Ihefu kusawazisha kupitia kwa Omar Mponda aliyeachia shuti kali la mguu wa kulia lililomshinda kipa Aishi Manula.

Kuanzia dakika ya 15 hadi dakika ya 23, safu ya ushambuliaji ya Ihefu ikiongozwa na Mponda sambamba na Joseph Kinyozi ilicharuka, lakini mashuti ya hatari takriban manne yaliokolewa na Manula.

Kwa ujumla bado kulionekana kutoelewana vema kwa Kennedy na Joash, lakini Mkenya huyo alijaribu kufuta makosa mengi kwa kucheza vizuri mipira ya juu kwa kichwa.

Hadi kipindi cha kwanza kinamalizika, Simba ilitoka kifua mbele huku ikimiliki zaidi mpira, lakini Ihefu ndiyo ilipiga mashuti mengi (matano) dhidi ya manne ya Simba yaliyolenga lango.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi, Ihefu ikitaka kusawazisha na Simba kuongeza, lakini mabeki wa pande zote walikuwa makini.

Dakika ya 65 Ihefu ilimtoa Jordan John na kumuingiza Samweli Jackson, huku dakika mbili baadaye Simba nayo ikimtoa Dilunga na kumuingiza Ibrahim Ajibu na Morrison akimpisha Kagere.

Kagere alifunga bao murua kwa kichwa dakika ya 74 akiitendea haki pasi ndefu ya Ajibu, lakini lilikataliwa baada ya mshika kibendera kuonyesha aliotea.

Kazi nzuri iliyofanywa na Bocco dakika ya 81 kutoka wingi wa kulia akimchambua Inno Kichiba ilishindwa kuzaa matunda baada ya Kagere kujigongagonda ndani ya 18.

Wakati huohuo, straika wa Namungo FC, Bigirimana Blaise amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga goli kwenye Ligi Kuu ya Tanzania Bara.

Bao la dakika ya 63 kwenye Uwanja wa Majaliwa mjini Ruangwa, lilimfanya mchezaji huyo raia wa Burundi kuweka rekodi hiyo, akiisaidia pia timu yake ya Namungo kupata ushindi wa bao hilo pekee dhidi ya Coastal Union kutoka Tanga.

Katika mechi nyingine za Ligi Kuu, Biashara United ilishinda bao 1-0 dhidi ya Gwambina FC, kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma.

Nayo Dodoma Jiji, imeanza vema, baada ya kuidungua Mwadui bao 1-0 kwenye mechi iliyochezwa Uwanja wa Jamhuri Dodoma.

Kwenye Uwanja wa CCM Gairo, timu ya Mtibwa Sugar imebanwa mbavu kwa kutoka suluhu bila kufungana dhidi ya Ruvu Shooting na kusababisha kugawana pointi moja moja kila moja.

# Nonga amtangazia Kagere vita ya kiatu

**Na Isaac Kijoti,** MBEYA

LICHA ya Paul Nonga msimu uliopita kumaliza akiwa na nusu ya mabao ya mfungaji bora wa Ligi Kuu Bara, Meddie Kagere wa Simba, straika huyo wa Gwambina FC, amemtangazia vita katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu.

Kagere msimu uliopita alicheka na nyavu mara 22, mabao ambayo yalimwezesha kutwaa kiatu hicho kwa msimu wa pili mfululizo.

Hata hivyo, Nonga ambaye ametua Gwambina FC iliyopanda Ligi Kuu msimu huu, mabao yake 11 aliyoifungia Lipuli FC msimu uliopita hayakuweza kuinusuru kushuka daraja.

Lakini mshambuliaji huyo, amesema msimu huu hatafanya kosa katika dhamira yake ya kuwania kutwaa kiatu hicho, kwa kuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu Bara.

Alisema anafahamu Kagere anafaidika zaidi kutokana na kuzungukwa na wachezaji wenye uwezo mkubwa kila upande katika kikosi cha Simba, lakini anaamini ataweza kutoa ushindani mkubwa kwake msimu huu.

"Nitapambana ili kuhakikisha ninampiku Kagere na wachezaji wengine katika mbio za kuwa mfungaji bora msimu huu.

"Najua mchezaji kama Kagere anafaidika zaidi kutokana na kuzungukwa na wachezaji bora katika kikosi chao, lakini naamini nikipambana naweza kumaliza kinara," alisema.

Mbio hizo za kuwania Kiatu cha Mfungaji Bora zilianza jana katika viwanja sita baada ya pazia la Ligi Kuu Bara kufunguliwa rasmi.

Wakati timu anayoichezea Kagere, Simba jana ikiwa mgeni wa Ihefu FC kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, Nonga na wachezaji wenzake wa Gwambina FC walikuwa ugenini dhidi ya Biashara United kwenye dimba la Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042